| | **Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo mwaka/Mwaka** | **634,368** | **251,567** | **634,368** | **760,784** |

### BAADHI YA MAELEZO KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA TAREHE 30 SEPTEMBA,2024

Hapo juu ni taarifa za Fedha za Benki zilizokaguliwa kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Septemba,2024 ambazo zimeandaliwa kulingana na viwango vya kimataifa vya uwasilishaji wa taarifa za fedha na matakwa ya sheria ya makampuni, Namba 12 ya mwaka 2002 CAP 212.

Taarifa hizi za Fedha zimekaguliwa na wakaguzi wa nje Auditax International - Certified Public Accountants (T) na kupata hati safi.

Yahya J. Kiyabo — **Tarehe**
**Meneja Mkuu** — 15/10/2024

Julius J. Sawaya — 15/10/2024
**Mkuu wa Fedha na utawala**

Aloyce Leonard — 15/10/2024
**Mkuu wa ukaguzi wa Ndani**

Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi, tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2016, na zinaonesha hali halisi.

Mohamed N. Mwinguku — **Tarehe**
**Mwenyekiti wa Bodi** — 15/10/2024

Mariam S. Mwanzalima — 15/10/2024
**Mjumbe wa Bodi**

### MINIMUM DISCLOSURE OF BANK CHARGES AND FEES

| | BANK CHARGES 2024 | | New Rates 2024 | |
|---|---|---|---|---|
| Sn | Transactions | Description | VAT Exclusive | VAT Inclusive |
| 1 | **Account Maintenance Fee** | | | |
| | Universal Savings | Per Month | Free | Free |
| | Individual Savings | Per Month | 2,500 | 2,950 |
| | Company Savings | Per Month | 13,000 | 15,340 |
| | **Group saving** | | - | - |
| | Amcos Collection | Per Month | 13,000 | 15,340 |
| | Amcos Business | Per Month | Free | Free |
| | Local council | Per Month | 13,000 | 15,340 |
| | Group saving | Per Month | 3,500 | 4,130 |
| 2 | **Min account Opening** | | | |
| | Universal Savings | Per Month | 5,000 | N/a |
| | Individual Savings | Per Month | 10,000 | N/a |
| | Company Savings | Per Month | 50,000 | N/a |
| | **Group saving** | | | |
| | Amcos Collection | Per Month | 50,000 | N/a |
| | Amcos Business | Per Month | 50,000 | N/a |
| | Local council | Per Month | 50,000 | N/a |
| | Group saving | Per Month | 20,000 | N/a |
| 3 | **Min operating Balance** | | | |
| | Universal Savings | Per Month | 5,000 | N/a |
| | Individual Savings | Per Month | 10,000 | N/a |
| | Company Savings | Per Month | 50,000 | N/a |
| | **Group saving** | | | |
| | Amcos Collection | Per Month | 50,000 | N/a |
| | Amcos Business | Per Month | 50,000 | N/a |
| | Local council | Per Month | 50,000 | N/a |
| | Group saving | Per Month | 20,000 | N/a |
| 4 | **Cash withdral Over the counter** | | | |
| | From TZS 1,000-4,999 | Per transaction | 300 | 354 |
| | From TZS 5,000-9,999 | Per transaction | 750 | 885 |
| | From TZS 10,000-19,999 | Per transaction | 1,200 | 1,416 |
| | From TZS 20,000-39,999 | Per transaction | 1,650 | 1,947 |
| | From TZS 40,000-49,999 | Per transaction | 2,000 | 2,360 |
| | From TZS 50,000-99,999 | Per transaction | 3,500 | 4,130 |
| | From TZS 100,000-199,999 | Per transaction | 4,500 | 5,310 |
| | From TZS 200,000-299,999 | Per transaction | 5,500 | 6,490 |
| | From TZS 300,000-599,999 | Per transaction | 6,500 | 7,670 |
| | From TZS 600,000-799,999 | Per transaction | 7,000 | 8,260 |
| | From TZS 800,000-999,999 | Per transaction | 7,500 | 8,850 |
| | From TZS 1,000,000-2,999,999 | Per transaction | 8,000 | 9,440 |
| | From TZS 3,000,000-4,999,999 | | 9,500 | 11,210 |
| | 5,000,000 - Above | | 9,500+0.12 % of excess max 170,000 | 9,500+0.12 % of excess max 170,000 |
| | Mwana A/C cash withdrawal exceeding 3rd transaction per annum | Per transaction | 3,000 | 3,540 |
| 5 | **Cash withdral - TACOBA Agency Banking** | | | |
| | From TZS 0-499 | Per transaction | 250 | 295 |
| | From TZS 500-999 | Per transaction | 250 | 295 |
| | From TZS 1,000-1,999 | Per transaction | 250 | 295 |
| | From TZS 2,000-2,999 | Per transaction | 300 | 354 |
| | From TZS 3,000-3,999 | Per transaction | 300 | 354 |
| | From TZS 4,000-4,999 | Per transaction | 300 | 354 |
| | From TZS 5,000-6,999 | Per transaction | 700 | 826 |
| | From TZS 7,000-9,999 | Per transaction | 700 | 826 |
| | From TZS 10,000-14,999 | Per transaction | 1,150 | 1,357 |
| | From TZS 15,000-19,999 | Per transaction | 1,150 | 1,357 |
| | From TZS 20,000-29,999 | Per transaction | 1,500 | 1,770 |
| | From TZS 30,000-39,999 | Per transaction | 1,500 | 1,770 |
| | From TZS 40,000-49,999 | Per transaction | 2,000 | 2,360 |
| | From TZS 50,000-99,999 | Per transaction | 3,200 | 3,776 |
| | From TZS 100,000-199,999 | Per transaction | 3,950 | 4,661 |
| | From TZS 200,000-239,999 | Per transaction | 5,300 | 6,254 |
| | From TZS 240,000-299,999 | Per transaction | 5,300 | 6,254 |
| | From TZS 300,000-399,999 | Per transaction | 6,500 | 7,670 |
| | From TZS 400,000-499,999 | Per transaction | 6,800 | 8,024 |
| | From TZS 500,000-599,999 | Per transaction | 7,500 | 8,850 |
| | From TZS 600,000-699,999 | Per transaction | 7,700 | 9,086 |
| | From TZS 700,000-799,999 | Per transaction | 8,000 | 9,440 |
| | From TZS 800,000-899,999 | Per transaction | 8,000 | 9,440 |
| | From TZS 900,000-999,999 | Per transaction | 8,500 | 10,030 |
| | From TZS 1,000,000-1,999,999 | Per transaction | 8,720 | 10,290 |
| | From TZS 2,000,000-2,999,999 | Per transaction | 8,720 | 10,290 |
| | From TZS 3,000,000-3,999,999 | Per transaction | 9,600 | 11,328 |
| | From TZS 4,000,000-4,999,999 | Per transaction | 9,600 | 11,328 |
| | From TZS 5,000,000-5,999,999 | Per transaction | 10,000 | 11,800 |
| | From TZS 6,000,000-6,999,999 | Per transaction | 11,000 | 12,980 |
| | From TZS 7,000,000-7,999,999 | Per transaction | 12,500 | 14,750 |
| | From TZS 8,000,000-8,999,999 | Per transaction | 14,000 | 16,520 |
| | From TZS 9,000,000-9,999,999 | Per transaction | 15,000 | 17,700 |
| | From TZS 10,000,000 & Above | Per transaction | 15,000 | 17,700 |
| 6 | **Activation of Dormant Accounts** | | | |
| | All other accounts | Free | Free | Free |
| | Saving account of personal loan customers | Per account | Free | Free |
| 7 | **Closing of Account** | | | |
| | Saving account | Per account | 5000 | 5900 |
| | All other accounts | Per account | 10000 | 11800 |
| 8 | **Inter-Bank (Outward Funds Transfer)** | | | |
| | TISS | Per transaction | 10000 | 11800 |
| | **Inter-Bank (Inward Funds Transfer)** | | | |
| | Internal Transfer | Per transaction | 1000 | 1180 |
| 9 | **Cards** | | | |
| | **New Cards** | | | |
| | Tacoba card | Per card | 5,000 | 5,900 |
| | Korosho card | Per card | 11,000 | 12,980 |
| | **New Cards due to expired** | | | |
| | Tacoba card | Per card | 5,000 | 5,900 |
| | Korosho card | Per card | 11,000 | 12,980 |
| | **Peplacement due to lost/spoiled** | | | |
| | Tacoba card | Per card | 10,000 | 11,800 |
| | Korosho card | Per card | 22,000 | 25,960 |
| | Annual card fee All Cards | per card | 10,000 | 11,800 |
| 10 | **Account statements** | | | |
| | Interim statement per month | per transaction | Free | Free |
| | Quartely statement | per transaction | 3,000 | 3,540.00 |
| | Adhoc from 4 up to 12 month | per transaction | 15,000 | 17,700.00 |
| | Adhoc above 12 month | per transaction | 20,000 | 23,600 |
| 11 | **Salary and Bulk payment** | | | |
| | Salary and Bulk payment fee | per transaction | 1,000 | 180 |
| | Transfer to other Banks | per transaction | 2,000 | 360 |
| | Balance enquiry | per request | Free | Free |
| 12 | **Information search** | | | |
| | For information up to 12 past months | per document | 50,000 | 59,000 |
| | For information of 1 to 5 past years | per document | 80,000 | 94,400 |
| | For information above 5 years | per document | 100,000 | 118,000 |
| | CCTV Image retrieve | Per request | 100,000 | 118,000 |
| 13 | **Introduction Letter and certificate of Balance** | | | |
| | Cerfificate of balance | per item | 50,000 | 59,000 |
| | status report | per report | 50,000 | 59,000 |
| | Visa recommendation | per item | 50,000 | 59,000 |
| | Any other introduction | per item | 50,000 | 59,000 |
| | Bank statement requested by other banks | per item | 50,000 | 59,000 |
| 14 | **Loan Fees** | | | |
| 1 | **MSE** | | | |
| | Loan Application fee | | 1% | |
| | Facility Fee | | 1% | |
| | Legal documentation fee | | 1% | |
| 2 | **AGRICULTURE LOANS** | | | |
| | Loan fee | 0-999,999 | 100,000 | 118,000 |
| | Loan fee | 1mn - 1,999,999 | 200,000 | 236,000 |
| | Loan Application fee | 2mn and above | 1% on Loan amount | |
| | Facility Fee | | 2% on Loan amount | |
| | Legal documentation fee | | 1% on Loan amount | |
| 3 | **PERSONAL LOAN** | | | |
| | Loan Application fee | | 0.55% MIN 55,000 | |
| | Facility Fee | | 1% MIN 90,000 | |
| | Legal documentation fee | | Free | |
| 4 | **GROUP LOAN** | | | |
| | Loan Application fee | | 1% on Loan amount | |
| | Facility Fee | | 2% on Loan amount | |
| | Legal documentation fee | | 1% on Loan amount | |
| 5 | **ASSET FINANCING LOAN** | | | |
| | Loan Application fee | | 1% on Loan amount | |
| | Facility Fee | | 1% on Loan amount | |
| | Legal documentation fee | | 0.5% on Loan amount | |
| 6 | **CHAPCHAP LOAN** | | | |
| | Loan Application fee | | Free | |
| | Facility Fee | | 0% | |
| | Legal documentation fee | | Free | |
| 15 | **charges on early loan payment** | | | |
| | Salary loan | | 5.9% min 500,000 | |
| | MSE business loan | | 3% on the unpaid amount min 500,000 | |
| | Agriculture loan | | Free | |
| | Other segment | | 3% on the unpaid amount | |
| | Restructuring Fee | | 2% min 150,000 | 177,000 |
| 16 | **Cheque Book order** | | | |
| | Per leaf - 100 | | 1,000 | 1,180 |




## HALMASHAURI YA JIJI LA DODOMA

## TANGAZO

Mkurugenzi wa Jiji la Dodoma anawatangazia wananchi ambao orodha yao ipo hapa chini waliolipia viwanja kwa nyakati tofauti eneo la Kikombo Kitalu "DA" na "N" kupitia benki, ila taarifa zao zinamapungufu ya majina, namba ya kiwanja na kitalu wafike ya Halmashauri iliyopo Manispaa ya zamani sehemu ya **mauzo ya viwanja** kwa ajili ya kuhakiki taarifa zao.

Muda wa utekelezaji ni kuanzia tarehe 28 Oktoba, 2024 hadi tarehe 10 Novemba, 2024.

Kushindwa kufanya hivyo, umiliki huo hautatambulika tena.

**ORODHA YA MAJINA YENYE TAARIFA PUNGUFU**

| NA | JINA | MALIPO |
|---|---|---|
| 1. | Christopher Kasung | 10,000.00 |
| 2. | Mbaga lyombe | 1,000,000.00 |
| 3. | Veisi Maineko | 42,000.00 |
| 4. | George Abel Ngab | 300,000.00 |
| 5. | Ngalawe Hassan Ramadha | 6,931,641.00 |
| 6. | Esther Mpangala | 5,000,000.00 |
| 7. | Victoria Mgala | 400,000.00 |
| 8. | Godfrey K. Msongwe | 9,096,340.00 |
| 9. | Eliaza Mangera Wangwe | 5,148,000.00 |
| 10. | Florence N. Kebwe | 2,515,000.00 |
| 11. | Ali Hussein Habib | 338,300.00 |
| 12. | Joseph Lukumbika | 265,000.00 |
| 13. | Rosina J Delima | 2,249,554.00 |
| 14. | Kelvin Mlambalamba | 1,200,000.00 |
| 15. | Starphod Marwa | 1,000,000.00 |
| 16. | Ally H. Thabit | 3,000,000.00 |
| 17. | Mariam Tawakel | 10,000.00 |
| 18. | Jeremia Baha | 255,000.00 |
| 19. | Shani Mwaruka | 400,000.00 |
| 20. | Ramadhan N Simba | 50,000.00 |
| 21. | Ally Habiba Thabit | 3,000,000.00 |
| 22. | Job Ndalo | 100,000.00 |
| 23. | Giligoli A Ndaro | 100,000.00 |
| 24. | Gloria Reuben Ndaro | 80,000.00 |
| 25. | Magreth W Luma | 10,000.00 |
| 26. | Chedi Ng'enda | 21,729,382.00 |
| 27. | Sospeter N Marco | 2,500,000.00 |
| 28. | Geophrey Mtweve | 1,150,000.00 |
| 29. | Leonary Kimario | 24,000.00 |
| 30. | Lilian Sebastian | 1,625,000.00 |
| 31. | Anna Elisamehe | 400,000.00 |
| 32. | Olais Peter | 300,000.00 |
| 33. | Mussa Deogratius Limb | 4,566,560.00 |
| 34. | Marium | 225,000.00 |
| 35. | Rainer | 4,607,934.00 |
| 36. | George | 100,000.00 |
| 37. | Jafari | 500,000.00 |
| 38. | Dann | 10,000.00 |
| 39. | Victoria | 1,015,000.00 |
| 40. | Jona | 50,000.00 |
| 41. | Alvin | 677,100.00 |
| 423. | Christina | 700,000.00 |
| 43. | Tina | 100,000.00 |
| 44. | Doreen | 300,000.00 |
| 45. | Kelvin | 1,500,000.00 |
| 46. | Innocent | 1,000,000.00 |
| 47. | Mabrouk | 100,000.00 |
| 48. | SHM | 1,000,000.00 |
| 49. | Khadija | 500,000.00 |
| 50. | Jackline | 40,000.00 |
| 51. | Zubeda | 100,000.00 |
| 52. | Kelvin | 250,000.00 |
| 53. | Antony | 180,000.00 |
| 54. | Stanley | 3,500,000.00 |
| 55. | Kelvin | 250,000.00 |
| 56. | | 2,000,000.00 |
| 57 | | 220,000.00 |
| 58. | | 4,447,406.00 |
| 59. | | 2,000,000.00 |
| 60. | | 5,000,000.00 |
| 61. | | 1,566,355.00 |

**Tangazo hili limetolewa na:**
**Mkurugenzi wa Jiji la Dodoma**


# Baba adaiwa kumnajisi bintiye

**Na Joctan Ngelly,**
GEITA

MAHAKAMA ya Wilaya ya Geita mkoani hapa, imeanza kusikiliza ushahidi wa kesi inayomkabili Mkazi wa Magogo, Fikili Masalu (38) kudaiwa kumnajisi bintiye (14) na kumsababishia maumivu makali mwilini.

Ni baada ya upande wa mashtaka kuiambia mahakama hiyo mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi wa Mahakama hiyo, Nyakato Bigirwa kuwa upelelezi wa kesi hiyo umekamilika.

Kabla ya kuanza kusikiliza ushahidi huo, Wakili wa Serikali, Deodatha Dotto alidai kuwa kati ya Januari 29 na Febuari 8, mwaka huu katika eneo la Magogo, mshtakiwa huyo alitenda kosa hilo kinyume cha sheria. Mshtakiwa huyo alikana shtaka hilo.

Wakili Dotto aliomba mahakama hiyo kusikiliza ushahidi wa shahidi mmoja wa upande wa Jamhuri aliyekuwa tayari kupanda kizimbani.

Hakimu Bigirwa alikubaliana na ombi hilo na kumruhusu shahidi hiyo kuanza kutoa ushahidi wake.

Shahidi huyo,Daktari wa Hospitali ya Halmashauri ya Mji wa Geita, Dk. Emmanuel Chambala (35) akiongozwa na Wakili Dotto, alidai kuwa Machi 5, mwaka huu akiwa kazini majira ya saa 9 mchana alifika mwalimu na mwanafunzi wake na kudai kuwa ana PF3 kutoka Kituo cha Polisi Wilaya ya Geita.

Dk. Chambala alidai kuwa Mwalimu huyo alimwomba amfanyie uchunguzi mwanafunzi huyo ili kuthibitisha kama ameingiliwa na baba yake.

Alidai alimfanyia uchunguzi kwa sehemu tatu, ya kwanza ukimwi, kaswende na mbegu za kiume.

Shahidi huyo aliendelea kudai kuwa baada ya kufanya uchunguzi alibaini mwanafunzi huyo hakuwa na bikira baada ya kuondolewa na kitu kigumu.

Alidai uchunguzi huo ulibaini kuwa mwanafunzi huyo hakuwa na maambikizi ya ukimwi wala kaswende.

Alidai baada ya kumaliza uchunguzi wake, alichukua PF3 na kuijaza na kumkabidhi mwalimu huyo ili waipeleke kituo cha polisi walikoitoa.

Baada ya Wakili Dotto kumaliza kumwongoza shahidi wake, Hakimu Bigirwa alimuuliza Wakili wa utetezi kama ana maswali ya kumuuliza shahidi huyo wa upande wa Jamhuri.

Wakili huyo alijibu ana maswali ya kumuuliza shahidi huyo wa upande wa Jamhuri, sehemu ya mahojiano yao ilikuwa kama ifuatavyo;

**Wakili:** Ili kuthibitisha hapa mahakamani kama wewe ni Daktari ni nini?

Shahidi: Ni namba yangu ya Baraza.

**Wakili:** Ni nani anasimamia uchunguzi?

**Shahidi:** Ni mpelelezi wa kesi.

**Wakili:** Binti alikuja na nani hapo hospitalini?

**Shahidi:** Binti alikuja na mwalimu wake.

**Wakili:** Kitu kigumu ni nini?

**Shahidi:** Kitu kigumu ni kitu chochote.

Baada ya Wakili wa utetezi Raulent Bugoti kumuuliza maswali shahidi huyo Hakimu Bigirwa alimuuliza Wakili wa Dotto kama ana maswali ya kusawazisha.

Wakili huyo alijibu hana na kuomba mahakama ipange tarehe nyingine kwa ajili ya kuendelea kusikiliza mashahidi wengine.

Hakimu Bigirwa aliahirisha kesi hiyo hadi Novemba 4, mwaka huu kwa ajili ya kuendelea kusikiliza mashahidi hao.

# Wataka mapambano magonjwa yasiyoambukiza kwa watu wote

**Na Mwandishi Wetu**

WANAOISHI na magonjwa yasiyoambukiza wameongoza wananchi katika matembezi ya hisani kutuma ujumbe kwa Watanzania kwamba, ni wakati kila mtu kushiriki vita ya magonjwa hayo kwa kuwa na mtindo bora wa maisha ili kunusuru vizazi vijavyo.

Mwenyekiti wa Chama cha Magonjwa Yasiyoambukiza Tanzania (TANCDA), Prof. Andrew Swai, alisema hayo mwishoni mwa wiki iliyopita wakati wa matembezi waliyoandaa na kufanyika kuanzia eneo la Coco Beach hadi makutano ya Barabara ya Aga Khan kisha kurudi Coco Beach, kwa lengo la kutuma ujumbe huo kwa Watanzania.

Prof. Swai ambaye ni Mwenyekiti wa Chama cha Wagonjwa wa Kisukari Tanzania (TDA), alisema matembezi hayo yamebebwa na kauli mbiu isemayo: "Ni muda sasa wanaoishi na magonjwa yasiyoambukiza na jumuiya kwa ujumla, kushiriki vita ya kupambana na magonjwa yasiyoambukiza."

**Alikumbusha jamii kwamba kuishi kwa kuzingatia mtindo bora wa maisha ni kula vyakula vya aina zote vinavyotakiwa kila siku ili kujenga na kuupa mwili nguvu.**

Alikumbusha jamii kwamba kuishi kwa kuzingatia mtindo bora wa maisha ni kula vyakula vya aina zote vinavyotakiwa kila siku ili kujenga na kuupa mwili nguvu.

Alisisitiza katika ulaji wa chakula mtu asizidishe kijiko kimoja cha chumvi kwa siku wala vijiko vitano vya sukari kwenye chakula kwa siku.

Mtaalamu wa Afya na Mazoezi kutoka TANCDA, Dk. Waziri Ndonde, alimpongeza Rais Samia kwa kuruhusu maeneo hayo wananchi kuyatumia kufanya mazoezi.

Alisisitiza umuhimu wa mazoezi ambayo ndio hujenga afya na kuhamasisha kila Jumamasi wana Dar es Salaam wahamasike kwenda maeneo hayo kushiriki kwa kutembea na kukimbia.

Kwa maoni: +255 677 020 701
Email: customerrelations@guardian.co.tz



Ukurasa 12

UCHAGUZI MSUMBIJI ULIVYOPITA...

**Frelimo imetwaa urais tena kwa kishindo, ikijibiwa kwa vurugu**





Ukurasa 13

**Rose alivyompambania mtotowa kike Mmaasai, sasa kuna viongozi**


# siasa

JUMATANO OKTOBA 30, 2024

Nipashe

HABARI BORA NA KAMILIFU


IKIWA UCHAGUZI MKUU LEO...

# Rais Samia akiongoza ulinzi SADC, Pinda akabidhiwa ukaguzi Botswana

• TAKUKURU nao wamo wamepiga kambi...

**Na Mwandishi Wetu**

LEO nchini Botswana kunafanyika uchaguzi mkuu nchini humo, kukiwapo wagombea Rais Mokgweetsi Masis, amekuwa uongozini nchini humo tangu 2019 baada ya kupata ushindi wa asimilia 51 ya kura zote.

Hadi sasa chama chake Botswana Democratic Party (BDP) kinatawala tangu uhuru kutoka Uingereza mwaka 1966, safari hii katika uchaguzi wa leo, anajinadi kwa ajenda ya chama chake "Tufanye mabadiliko pamoja na tujenge ufanisi kwa wote."

Anachuana na kiongozi wa umoja wa wapinzani; Duma Boko kutoka Chama Umbrella for Democratic Change (UDC), Dumelang Saleshando wa Botswana Congress Party (BCP) na Mephato Reatile, anayetoka Botswana Patriotic Front (BPF).

Hiyo inaendelea, huku Tanzania ikibeba heshima kipekee, Waziri Mkuu mstaafu Mizengo Pinda, anaongoza Misheni ya Uangalizi wa Uchaguzi ya Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (SADC-SEOM) na wapo nchini humo tangu wiki iliyopita.

Ni mwendelezo wa heshima tajwa, kwani Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, naye tangu mwezi Agosti anaongoza chombo cha ulinzi na usalama SADC, chenye wajibu wa kuhakikisha kunakuwapo uchaguzi bora katika nchi hiyo mwanachama wake.

Ijumaa iliyopita, Pinda na timu yake wamekutana na Rais wa nchi hiyo kujitambulisha, Mokgweetsi Masisi, katika ofisi yake jijini Gaborone, pia kupata ufafanuzi wa kidemokrasia na maendeleo nchini Botswana.

Waziri Mkuu huyo mstaafu wa Tanzania na timu yake, walitumia ziara hiyo kufafanua wajibu wa kama anayoiongoza kulingana na misingi na mwongozo wa SADC kuhusu uchaguzi wa kidemokrasia, akimhakikishia Rais huyo utayari walio nao katika kufanikisha uangalizi katika uchaguzi mkuu wa leo Botswana.



Waziri Mkuu mstaafu, Mizengo Pinda, akiwa na timu ya wakaguzi wa uchaguzi wa SADC, katika uchaguzi mkuu wa Botswana, walipokutana viongozi wa kisiasa nchini humo. **PICHA: MTANDAO**

Tangu wikiendi iliyopita, Pinda na timu yake walishakutana na wadau, ambao ni Tume Huru ya Uchaguzi ya Botswana (IEC), Kamishna wa Polisi wa Botswana, Wizara ya Mambo ya Nje, viongozi wa vyama vya kisiasa, taasisi zisizo za kiserikali husika, na mabalozi wanaowakilisha Botswana na SADC.

Pia, timu hiyo ilipitia vyombo vya habari na mitandao ya kijamii, kupata ufahamu kuhusu yanayohusiana na uchaguzi mkuu ujao wa nchi hiyo.

Katika mazungumzo yao, Rais Masisi, akauambia ugeni huo waangalizi, kwamba: "Nendeni mkazungumze na yeyote mnayefikiri anaweza kuwasaidia nyinyi na timu yenu kufanya kazi zenu vizuri. Botswana ni nyumbani kwa SADC."

Pia, mkuu huyo wa nchi ambaye ni mgombea urais, akaahidi kila kitu kitakuwa sawa leo na uchaguzi utakuwa huru, haki wa kuaminika, pia na usalama na amani.

Mnamo Septemba mwezi uliopita, Rais Dk. Samia, ambaye ni Mwenyekiti wa Asasi ya Siasa Ulinzi na Usalama ya SADCm walimteua Pinda, kuongoza Misheni ya Uangalizi wa SADC katika Uchaguzi Mkuu wa Botswana.

Chombo anachoongoza Pinda huko Botswana, kinajumuishwa na maofisa kutoka SADC, wanachama wa taasisi hiyo ya SADC kutoka Malawi, Zambia, Tanzania na Baraza la Ushauri la Uchaguzi la SADC (SEAC).

Nafasi ya Rais Dk. Samia, alipata kupitia Mkutano wa Kawaida wa 44 wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa SADC, mnamo Agosti 17 mwaka huu, kuongoza jukumu la uenyekiti wa Asasi ya Ushirikiano wa Siasa, Ulinzi na Usalama.

Ni chombo chenye jukumu la kusimamia ulinzi na usalama katika ukanda wa SADC, ikitoa ushauri kwa nchi wanachama kuhusu masuala yanayohatarisha amani, usalama na utulivu katika kanda hiyo.

Katika majukumu yanayoratibiwa katika ngazi ya wakuu wa nchi na serikali wa asasi hiyo, nafasi yake hufuata mzunguko, kama ilivyo katika uongozi wa juu wa SADC.

Hata hivyo, kigezo cha kuongoza nafasi hiyo anayotumikia sasa Rais Dk. Samia, inagusa kigezo cha kuwapo hali ya ulinzi na usalama katika nchi hiyo anakotoka mwenyekiti mteule.

Tanzania imeshawahi kuwa mwenyekiti mara tatu katika vipindi tofauti: 2006/2007; 2012/2013; na 2016/2017 na sasa itaongoza kwa kipindi cha 2024/2025, ikiwa mwenyeji wa vikao vya asasi hiyo kwa kipindi husika.

Kwa sasa, chombo anachoongoza Rais Dk. Samia, kina wanachama Zambia (Mwenyekiti aliyemaliza muda) Tanzania (Mwenyekiti wa sasa) na Malawi (Makamu Mwenyekiti).

Hadi sasa inatajwa miongoni mwa majukumu makubwa mbele ya chombo hicho, yanajumuisha kusimamia amani Mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DRC).

**TAKUKURU MKUTANONI**

Viongozi wa TAKUKURU Kurugenzi ya Uchunguzi, Thobias Ndaro na Alexander Kuhanda, wamekuwa wakihudhuria mafunzo maalum yanayoendeshwa na SADC nchini Botswana kuanzia Oktoba 17 hadi 20, mwaka huu.

Mafunzo hayo yanafanyika ikiwa ni sehemu ya maandalizi kwa ajili ya uangalizi wa uchaguzi mkuu nchini humo unaotarajiwa kufanyika Oktoba 30, 2024 ambao Tanzania inaungana na nchi nyingine mwanachama wa SADC katika zoezi hilo la uangalizi.

Pamoja na Tanzania, nchi nyingine zilizotuma waangalizi ni Zambia, Malawi, DRC, South Africa, Zimbabwe, Namibia, Msumbiji, Eswatin na Lesotho

UCHAGUZI MSUMBIJI ULIVYOPITA...

# Frelimo imetwaa urais tena kwa kishindo, ikijibiwa kwa vurugu

**Na Christina Mwakangale**

CHAMA tawala nchini Msumbiji, FRELIMO, kimetangazwa kushinda uchaguzi uliogubikwa na mgawanyiko, ghasia na hata baadhi ya maeneo ya umma kuchomwa moto.

Hadi sasa chama hicho kimedumu madarakani kwa takribani miongo mitano na miongoni mwa taifa lililoko kusini mwa Afrika, kudumu mamlakani kwa muda mrefu zaidi.

Wiki iliyopita, Tume ya Taifa ya Uchaguzi Msumbiji (CNE) ilitangaza ushindi wa Daniel Chapo, anayetokea chama hicho cha Frelimo.

Frelimo kimedumu madarakani tangu mwaka 1975. Chapo kupitia chama hicho amepata kura asilimia 70.67 kwenye uchaguzi mkuu wa urais uliofanyika Oktoba 9, mwaka huu.

Mpinzani wake Venâncio Mondlane, kutoka chama cha Optimist Party for the Development of Mozambique (Podemos), ameshika nafasi ya pili akiwa na asilimia 20.32 ya kura zilizopigwa katika kiti hicho.

Amepinga ushindi huo na kutoyatambua matokeo hayo, ambayo bado yanapaswa kuthibitishwa na kutangazwa na Baraza la Katiba.

Kwa mujibu wa CNE, Frelimo pia imejiimarisha kwenye wingi wa idadi ya wabunge, ikiongezeka kutoka 184 hadi manaibu 195 (kati ya 250) na ikachagua magavana wote 10 wa majimbo ya nchi hiyo.

Mwishoni mwa wiki, wakuu kadhaa wa nchi wakiwamo wa Afrika Kusini, Zimbabwe, Tanzania na Venezuela, pamoja na serikali ya China, walimpongeza Rais Mteule, Daniel Chapo.

Uchaguzi Mkuu wa Oktoba 9 mwaka huu, ni wa saba wa Rais wa sasa anayeondoka madarakani nchini, Filipe Nyusi, akiwa amefikia kikomo cha mihula miwili.

Siku ya Alhamisi iliyopita kabla ya kutangazwa matokeo ya jumla, Rais wa CNE, Carlos Matsinhe, akasema kwamba wakati wa siku ya kupiga kura na mchakato wa kuhesabu kura, kesi kadhaa za utata zilianzishwa katika mahakama pamoja na baadhi ambazo zilipelekwa kwenye Baraza la Katiba.

“Michakato hiyo inatarajiwa kusababisha uamuzi sahihi. Hata hivyo, CNE inatakiwa kisheria kutangaza matokeo ya kura ndani ya siku 15, baada ya kupiga kura. Hatukuweza kusubiri maamuzi ya migogoro hii inayoendelea,” anasema Matsinhe na kuongeza:

“Kutangazwa kwa matokeo hakumalizi mchakato mzima, hadi matokeo yatakapothibitishwa na washindi kutangazwa.”



Mshindi wa kiti cha urais nchini Msumbiji, Daniel Chapo, alipokuwa katika harakati za kampeni. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

“Michakato hiyo inatarajiwa kusababisha uamuzi sahihi. Hata hivyo, CNE inatakiwa kisheria kutangaza matokeo ya kura ndani ya siku 15, baada ya kupiga kura.



Wafuasi wa chama kikuu cha upinzani, Renamo, wakifurahia jambo katika harakati za uchaguzi nchini Msumbiji.

Baada ya hesabu ya kati katika ngazi ya wilaya 154 na kisha mikoani, CNE ilikuwa na siku 15 kutangaza matokeo rasmi na sasa ni juu ya Baraza la Katiba nchi hiyo kutangaza matokeo, baada ya kuhitimisha uchambuzi wa matokeo.

Rufani kutoka kwa wagombea na vyama vya upinzani, pia zipo.

Mbali na Mondlane, mgombea urais wa chama National Resistance (Renamo), ambacho ni chama kikuu cha upinzani cha sasa), Ossufo Momade, akiwa mmoja wa wagombea wanne wa urais, akasema ‘hatambui matokeo ya uchaguzi yaliyotangazwa na CNE na akataka kura zipigwe kubatilishwa.”

Mgombea urais, Lutero Simango, kupitia chama cha Democratic Movement of Mozambique (MDM), pia akayakataa matokeo, akidai yameghushiwa katika sekretarieti na kuahidi hatua za kisiasa, pia kisheria.

Kutangazwa matokeo na CNE kulisababisha maandamano na mapigano na polisi nchini Msumbiji, hasa jijini Maputo, dhidi ya waandamanaji wanaomuunga mkono Mondlane.

Kwa mujibu wa jeshi la polisi wa nchi hiyo, watu 10 waliuawa, kundi lingine likijeruhiwa na takribani 500 wakishikiliwa.

### MJUE MGOMBEA CHAPO

Daniel Chapo, mgombea urais wa Frelimo aliyejulikana sana, anaonekana kuwa wakala wa mabadiliko, akichukua nafasi ya Filipe Nyusi, ambaye amehudumu kwa mihula miwili.

Akiwa na umri wa miaka 47, Chapo, amepata asilimia takribani 71 ya kura, atakuwa rais wa kwanza kuzaliwa baada ya uhuru wa Msumbiji huru ya mwaka 1975, mpinzani wake wa karibu, Venancio Mondlane amepata asilimia 20 ya kura zote.

Uchaguzi huo umekumbwa na madai ya wizi wa kura na mauaji ya wafuasi wa upinzani, hivyo kusababisha maandamano nchini kote.

Rais wa Zimbabwe, Emerson Mnangagwa, ambaye pia alikumbwa na madai ya udanganyifu katika uchaguzi kwa miaka mingi, amempongeza Chapo kwa ushindi wake, akiuita ‘ni mkubwa’, hata kabla ya matokeo kutangazwa.

Kundi la zamani la waasi la Renamo, sasa chama kikuu cha upinzani, kimeshika nafasi ya tatu. Tume ya uchaguzi inasema asilimia 43 ya wapiga kura ambao ni zaidi ya milioni 17, walijisajili kushiriki katika uchaguzi huo.

Kwa mujibu wa chombo cha habari cha Club of Mozambique, maandamano yaliyoongozwa na vijana huko Chalaua, Moma, Nampula, polisi ya wilaya ya Moma ilitumia nguvu ambazo hazingeweza kuzuia maandamano hayo.

Maofisa wote wa polisi waliotumwa kurejesha utulivu walikimbia na amri ya eneo hilo ikachomwa moto, kutia ndani pikipiki na gari la polisi.

Wakazi wa Chalaua wanasema kuwa watu hao walinaswa bunduki na aina ya AK 47 iliyotelekezwa na polisi. Nyumba za kamanda, mkuu wa wadhifa wa utawala na makao makuu ya chama cha Frelimo, pia zilichomwa moto.

Operesheni zilianza, huku watu wakitambua nyumba za maofisa wa polisi wa eneo hilo. Polisi walikuwa wamekimbia wote na hakukuwa na taarifa za nyumba za polisi mmoja mmoja kuchomwa moto.

Hapakuwapo matukio ya risasi na hakuna mashambulizi ya polisi na waandamanaji waliwakomboa wafungwa wao wote.

Chama cha Podemos, kiliwasilisha rufani, kwa Baraza la Katiba, kupinga matokeo ya uchaguzi mkuu nchini Msumbiji, baada ya kufanyika Oktoba 9 mwaka huu, madai yao ni kwamba mgombea Venâncio Mondlane, alishinda uchaguzi wa urais.

“Tunawasilisha hesabu yetu inayolingana,” alielezea Dinis Tivane, kutoka chama Podemos, baada ya kuwasilisha rufani kwenye Baraza la Katiba Jumapili, iliyopita, akidai kwamba baada ya kuhesabu karibu asilimia 70 ya dakika za awali na notisi zilitoa majibu ushindi kwa asilimia 53.30 kwa Venâncio Mondlane.

# Rose Njiro alivyompambania mtoto wa kike Mmaasai, sasa kuna viongozi

• Awaingiza shule, leo wasikika na kukubalika • Aaanika ujanja aliyopitia, akivuka magumu • Serikali 'yakoshwa' yaungana na juhudi zake

***JUMATANO iliyopita ilikuwa na simulizi ya chungu na tamu ya safari ya ukombozi wa mtoto wa kike wa Kimaasai, ndani ya magumu ya utamaduni wao, haki na fursa za kukubalika katika jamii yake ni mtihani mgumu. Endelea na simulizi ya ukaguzi wa mwandishi...***



Rore Njiro, akizungumza na baadhi ya wasichana waliokimbia kuozeshwa, wanaosaidiwa katika kituo chake kilichoko Moshono, mkoani Arusha. **PICHA: ELIZA ZAYA**

ROSE Njiro (40), anaisimulia Nipashe kuwa pamoja na kupambana kuvunja mila hiyo kandamizi kwa wanawake katika jamii hiyo ya Kimaasai, nguvu nyingine aliitumia kuimarisha kuhakikisha watoto wa kike wanapelekwa shule.

Anasema kwenye jamii hiyo ya Kimaasai, watoto wa kike walikuwa hawaruhusiwi kwenda shule, lakini alipambana kushawishi kuhakikisha wanaandikishwa na kwenda kusoma.

"Zamani ilikuwa kwamba, mwezi wa kwanza wakati watoto kuandikishwa shule, kilikuwa kinakaa kikao cha kijiji, ili waamue mtoto gani apelekwe na hapo wa kike hahesabiki kwenda shule. Kwa hiyo niliamua kuanzisha chekechea katika Kata ya Loliondo (Arusha) na nilienda kwa ujanja ili niwapate watoto wa kike.

"Niliwaambia wazee wa mila kwamba, nataka nijenge Shule ya Kiingereza na nikawaambia kwamba baba yeyote wa familia atakayekubali kuniletea wasichana wawili au watatu kwenye shule ya chekechea, nitamsaidia kusomesha mtoto wa kiume mmoja bure.

"Kwa hiyo walianza kuleta watoto wa kike na nikapata wengi, lakini wakati huo kule shule za serikali hawapeleki watoto, hawaamini katika elimu, bali wanaamini kwamba mifugo ndio kila kitu.

"Ilibidi hadi Ofisa Elimu baada ya kusikia nimepata watoto wengi wa kike waliojiandikisha kuja shule, aje aniulize nimetumia mbinu gani kuwapata hao watoto maana kule kwao hawapelekwi.

"Lengo la kutumia njia hiyo, ndio ilikuwa ujanja wangu ili wakitoka hapo waende darasa la kwanza na waanze kusoma moja kwa moja. Kwa kweli mbinu hiyo ilifanikiwa na baadaye, ile shule niliyojenga ndio ilisababisha kujengwa shule nyingine nyingi za awali Loliondo na Wilaya ya Ngorongoro.

"Nikawa nawaambia, faida za mtoto wa kike na tangu pale wakaanza kuwaruhusu watoto wa kike kwenda shule na mpaka sasa wanaofika hadi vyuo vikuu. Zamani hata watoto wa kiume wenyewe waliokuwa wakipekwa shuleni ilikuwa ni kama adhabu kwao, yaani aliyekuwa akipelekwa shuleni ni mtoto wa mwanamke ambaye hapendwi na mume wake.

"Kwa hiyo, alikuwa akipelekwa kusoma ni kama kumkomoa, kwa sababu walikuwa wanaamini yule anayeachwa kufuga ndio mwenye thamani zaidi," anasimulia.

## UMASAINI LEO

Rose anaeleza kwamba, mpaka sasa watoto wa kike waliopita kwenye mikono yake kwa kuwasimamia kidete wapate elimu ambao wengine wako vyuo vya kati na vyuo vikuu jumla yao 124.

Rose ana maelezo kwamba, kulivyo sasa baada yeye kutoa elimu hiyo, hali imebadilika, jamii imeanza kuamini katika mawazo ya wanawake yameanza kusimama kwenye vikao vya vijiji na hata katika mikutano ya hadhara.

Anafafanua, mawazo yao sasa yanaheshimika zaidi, kuliko ya wanaume, kwa sababu wao wanaposimama wanazungumza ukweli wa yale wanayopinga.

Kwa mujibu wa Rose, mara nyingi wao kinamama ndio wanakuwa wanabaki na familia hasa wanaume wanaposafiri, kwenda kulisha mifugo.

"Kwa mfano kwenye migogoro ya ardhi ikiwamo Pori Tengefu la Loliondo na migogoro mingine mingi, wanawake ndio wamekuwa wakisimama na kutetea hoja kwa sababu sasa hivi wao ndio wanaonekana wamejaliwa hekima namna ya kuwasilisha na siyo wana laana tena.

"Sasa hivi wanaonekana wamejaliwa lugha ya unyenyekevu, kwa hiyo inapokuja masuala magumu kama hayo, kwa sasa wanawatanguliza mbele wanawake ndio wazungumze.

"Kwa hiyo, kwa sasa wanaume wameanza kurudi kwangu, wananipongeza na kunipa majina mazuri wakati hao hao ndio walikuwa wananirushia mawe na kunibatiza majina mabaya," anasimulia Rose.

## VIONGOZI WA KIKE

Rose anasema baada ya kuona elimu aliyowapatia imeanza kueleweka, alianza kupenyeza ajenda ya nyingine ya kupata viongozi wa kike kimila, akiwaona kwa wazee wa mila.

"Mabadiliko hayo yaliyoanza kuonekana, yalinisaidia kunipa nafasi ya kuingia kwenye vikao vya viongozi hao wa mila (Malaigwanani), nikaanza kufanya nao mikutano, kuwahamasisha wamwamini mwanamke.

"Kwa sababu sisi wote tumezaliwa na wazazi, kwa hiyo maumbile yetu yasitufanye sisi hatufai, nikawaambia kwamba hata vitabu vitukufu vya Mungu havitaki ubaguzi, nikaendelea kuwahamasisha ili kuvunja ile mitazamo yao hasi kwa mwanamke.

"Ilinichukua muda mrefu mpaka kuwaaminisha na kuwashawishi wamwamini mwanamke na kumpa nafasi kwa sababu si rahisi kitu ambacho wameamini katika maisha yao, kiwatoke mara moja.

"Nilienda nao taratibu hivyo hivyo, wanakwenda wanaamini wachache, hivyo hivyo naendelea kuwashika, na nikawa nawakutanisha viongozi hao wa mila na vyombo vya dola, Jeshi la Polisi, TAKUKURU, wakuu wa idara wa halmashauri, ustawi wa jamii.

"Baadhi ya wanawake ambao ni viongozi katika nyanja mbalimbali serikalini na kwenye taasisi, nawachanganya humo" anaeleza Rose, akinena lengo la kufanya hivyo, ni kuiteka jamii yake ielewe watu wote ni muhimu na wanategemeana.

"Nilikuwa nawakutanisha na wanawake viongozi kutoka katika nyanja tofauti, ili wajifunze na waone kwamba mbona hawa ni wanawake na wanaongoza, kwanini isiwe katika jamii yetu, nikitaka waone kwamba sisi sote ni viungo vinavyotegemeana.

## VIONGOZI WA KIKE

"Baada ya kuona kwamba wameanza kunielewa, ikabidi nianze kuwadadisi kwamba kwa nini huwa hakuna viongozi wanawake wa mila. Nikaanza tena kuwaelimisha na kwa sababu tayari wameanza kuelewa kwamba mwanamke ana uwezo.

"Ikabidi na wao wakae wazungumze na wakaja na tamko mwaka jana 2023 kwamba, wamebariki kuwapo na viongozi wa kike kwenye jopo la viongozi wa kimila.

"Mwaka huu Julai tukawasimika wanawake sita (Mangaigwanani) kuingia kwenye jopo hilo la viongozi wa kiume wa kimila (Malaigwanani) na kulikuwa na sherehe kubwa kusherehekea jambo hili kubwa la kihistoria ambalo halijawahi kutokea tangu jamii hii iundwe.

"Na sherehe ziligharimiwa na viongozi wa kiume wenyewe wa kimila na ndio walitangaza rasmi kwamba sasa mwanamke anaruhusiwa kuwa kiongozi na atakuwa na uwezo wa kusimama mahali popote kwenye nyanja ya uongozi iwe wa kimila au serikali.

"Katika sherehe hizi za kuwasimika wanawake viongozi wa kimila, viongozi wa serikali nao walialikwa. Ilikuwa ni gumzo na mshangao mkubwa kwa jamii ya kimaasai kumkubali mwanamke lakini ndio ikawa imekuwa.

"Kwa hiyo, kwa sasa tuna wanawake viongozi kutoka ata sita za wilaya ya Ngorongoro ni mapinduzi ya kihistoria yamefanyika," anasema Rose.

Anafafanua kuwa, kwa sasa wanawake ndio wanaowatumia kuwahamasisha kinamama wenzao kusimama kwenye nafasi za uongozi kwa kuanzia katika uchaguzi wa mwaka huu wa serikali za mitaa.

Hapo anarejea kwamba, hadi sasa wana orodha kubwa mpaka ya wanawake waliojiandikisha kugombea katika nafasi ya uchaguzi ujao wa serikali za mitaa mwaka huu.

## HAKI YA KURA

Rose anasema zamani mwanamke wa jamii ya kimaasai alikuwa hana uamuzi na kura yake, alikuwa analazimishwa achague yule ambaye mume wake anataka na kura haikuwa siri kwa upande wake.

Lakini sasa, nalo wamewaelimisha na wameacha kuwalazimisha kuchagua watu wasiowataka. Anafafanua:

"Zamani mwanamke wa Kimaasai huna uamuzi na kura yako, sehemu ambayo mume wako anapita, ndio hapohapo na wewe unatakiwa upite, hata kama hutaki, na ilikuwa hakuna siri unaambiwa utamke kwa sauti ili wasikie je umeenda tofauti na mume wako?

"Lakini sasa, wamejua haki zao, sasa hivi wanawake wanasema kura ni siri, hutakiwi kupiga kwa sauti na unamchagua unayemtaka siyo kuchaguliwa na mtu, kwa hiyo sasa hivi wamejua kura ni haki yao."

***• Inaendelea Jumatano ijayo.***

MKOMBOZI COMMERCIAL BANK

a bank with integrity

# MKOMBOZI COMMERCIAL BANK PLC

# UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA

## Imetolewa chini ya kanuni ya 7 na ya 8 ya Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2014

### WARAKA MIZANIA KWA TAREHE SEPTEMBA 2024
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo Mwaka ya /Mwaka wa sasa 30/09/2024 | Robo Mwaka ya /Mwaka Uliopita 30/06/2024 |
|---|---|---|---|
| A. | MALI | | |
| 1 | Fedha Taslimu | 6,087 | 7,160 |
| 2 | Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | 16,747 | 16,895 |
| 3 | Uwekezaji Katika Amana za Serikali | 55,177 | 57,138 |
| 4 | Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 5,839 | 12,963 |
| 5 | Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | 104 | 92 |
| 6 | Miamala Baina ya Matawi | - | 9 |
| 7 | Bili Zilizoafikiwa | - | - |
| 8 | Dhima za Wateja Zilizokubalika | - | - |
| 9 | Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | 13,886 | 9,478 |
| 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | - | - |
| 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 156,695 | 143,605 |
| 12 | Mali Nyingine | 10,240 | 9,645 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | 539 | 539 |
| 14 | Akaunti za udhamini | - | - |
| 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 14,178 | 13,782 |
| 16 | **JUMLA YA MALI** | **279,492** | **271,306** |
| | | | |
| **B. DHIMA** | | | |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | - | - |
| 18 | Amana za Wateja | 213,008 | 214,151 |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | - | - |
| 20 | Amana Maalumu | - | - |
| 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | - | - |
| 22 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | 6 | 6 |
| 23 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 7,158 | 4,875 |
| 24 | Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | - | - |
| 25 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | - | - |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa | 9 | 9 |
| 27 | Dhima Nyingine | 8,989 | 10,703 |
| 28 | Madeni | 7,268 | 4,200 |
| 29 | **JUMLA YA DHIMA** | **236,438** | **233,944** |
| 30 | **MALI/(DHIMA) HALISI (16 kutoa 29)** | **43,054** | **37,362** |
| C. | **FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 23,555 | 23,555 |
| 32 | Akiba ya Mtaji | 7,476 | 5,423 |
| 33 | Mapato Yaliyobakizwa | 3,435 | 3,435 |
| 34 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | 9,763 | 6,124 |
| 35 | Akaunti Nyingine za Mtaji | (1,175) | (1,175) |
| 36 | Stahiki ya Wenyehisa Chache | - | - |
| 37 | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **43,054** | **37,362** |
| 38 | Dhima Zisizo Dhahiri | 3,573 | 5,587 |
| 39 | Mikopo Chechefu | 8,650 | 9,079 |
| 40 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 2,560 | 2,778 |
| 41 | Mali Nyingine Chechefu | - | - |
| D. | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| (i) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 15% | 14% |
| (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 5% | 6% |
| (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 75% | 68% |
| (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 57% | 54% |
| (v) | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 81% | 77% |
| (vi) | Ongezeko la Amana | -1% | 3% |
| (vii) | Ongezeko la Mali | 3% | 4% |

### TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA SEPTEMBA 2024
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo ya Mwaka sasa 30/09/2024 | Robo ya mwaka Linganishi mwaka uliopita 31/09/2023 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 30/09/2024 | Limbikizo la Mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) 30/09/2023 |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | |
| 1 | Mapato ya Riba | 9,684 | 6,669 | 25,600 | 18,512 |
| 2 | Gharama za Riba | (1,699) | (1,830) | (5,080) | (5,451) |
| 3 | **Mapato Halisi ya Riba (1kutoa 2)** | **7,986** | **4,838** | **20,521** | **13,061** |
| 4 | Madeni Viza Yaliyofutwa | - | - | - | - |
| 5 | Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | **(786)** | (472) | **(1,803)** | (1,419) |
| 6 | **Mapato Yasiyo ya Riba:** | **1,739** | **2,864** | **5,202** | **7,322** |
| | 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | 422 | 724 | 1,845 | 1,763 |
| | 6.2 Ada na Kamisheni | 1,112 | 1,569 | 2,767 | 4,302 |
| | 6.3 Gawio | - | - | - | - |
| | 6.4 Mapato Mengine | 205 | 571 | 591 | 1,257 |
| 7 | **Gharama Zisizo za Riba:** | **(5,299)** | **(4,530)** | **(14,157)** | **(12,417)** |
| | 7.1 Mishahara na Mafao | (2,205) | (2,191) | (6,821) | (6,534) |
| | 7.2 Ada na Kamisheni | - | - | - | - |
| | 7.3 Gharama Nyingine | (3,094) | (2,339) | (7,336) | (5,883) |
| 8 | **Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | **3,639** | **2,700** | **9,763** | **6,547** |
| 9 | Tengo la Kodi ya Mapato | - | - | - | - |
| 10 | **Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **3,639** | **2,700** | **9,763** | **6,547** |
| 11 | **Mapato Mengine Yaliyojumuishwa (bainisha)** | - | - | - | - |
| 12 | **Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka** | **3,639** | **2,700** | **9,763** | **6,547** |
| 13 | Idadi ya Waajiriwa | 195 | 183 | 195 | 183 |
| 14 | Mapato kwa Hisa | 154 | 115 | 414 | 278 |
| 15 | **Idadi ya Matawi** | **13** | **12** | **13** | **12** |
| | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | | |
| (i) | Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | 1% | 1% | 1% | 1% |
| (ii) | Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | 9% | 3% | 6% | 6% |
| (iii) | Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 46% | 48% | 50% | 48% |
| (iv) | Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 15% | 3% | 9% | 7% |

### TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO/MWAKA ULIOISHIA SEPTEMBA 2024
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo Mwaka ya sasa 30/09/2024 | Robo iliyopita 30/06/2024 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 30/09/2024 | Limbikizo la Mwaka Linganishi 30/09/2023 |
|---|---|---|---|---|---|
| I: | Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za | | | | |
| | **Mapato/(Hasara) Halisi** | 3,639 | 3,020 | 9,763 | 6,547 |
| | Marekebisho kwa Ajili ya: | | | | |
| | - Hasara Katika Mali | 786 | 888 | 1,803 | 1,419 |
| | - Badiliko Halisi Katika Mikopo | (13,090) | (3,588) | (22,434) | (11,951) |
| | - Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | - | - | - | - |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana | (1,143) | 5,918 | 5,611 | 11,553 |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi | | | | |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | 569 | 979 | 2,513 | (57) |
| | -Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | (607) | (2,787) | (3,738) | (1,719) |
| | - Kodi Iliyolipwa | (679) | (679) | (679) | (48) |
| | - Mengineyo (bainisha) | - | - | - | - |
| | **Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji** | **(10,525)** | **3,751** | **(7,161)** | **5,744** |
| II: | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | | | | |
| | Gawio Lililopokewa | - | 11 | 11 | 10 |
| | Ununuzi wa Mali za Kudumu | (649) | - | (1,783) | (1,954) |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | - | - | - | - |
| | Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na | - | - | - | (8,721) |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana | | | | 1,351 |
| | Mengineyo (bainisha) | (2,454) | (399) | (8,684) | 2,834 |
| | **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji** | **(3,103)** | **(388)** | **(10,456)** | **(6,479)** |
| III: | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha:** | | | | |
| | Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda | - | - | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | - | - | - |
| | Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | - | - | - | - |
| | Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | 3,068 | 0 | 2,757 | 2,008 |
| | Mengineyo (bainisha) | - | - | - | - |
| | **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Kifedha** | **3,068** | **0** | **2,757** | **2,008** |
| | | | | | |
| IV: | **Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha** | | | | |
| | Ongezeko / Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na | **(10,560)** | **3,364** | **(14,860)** | **1,273** |
| | Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | 33,661 | 30,298 | 37,962 | 41,409 |
| | **Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo Mwaka/Mwaka** | **23,102** | **33,661** | **23,102** | **42,682** |

| | | Robo Mwaka ya 30-Sep-24 | Robo Mwaka ya 30-Jun-24 |
|---|---|---|---|
| | **A. MALI** | | |
| 1 | Fedha taslimu | 3,367 | 4,274 |
| 2 | Salio katika Benki Kuu ya Tanzania | 11,003 | 10,249 |
| 3 | Uwekezaji katika amana za Serikali | 90,036 | 89,992 |
| 4 | Salio katika benki nyingine na taasisi za fedha | 4,332 | 10,083 |
| 5 | Hundi na miamala ya kushughulikiwa | - | - |
| 6 | Miamala baina ya matawi | - | - |
| 7 | Bili zilizoafikiwa | - | - |
| 8 | Dhima za wateja zilizokubalika | - | - |
| 9 | Mikopo iliyotolewa kwa benki nyingine | 10,724 | 2,594 |
| 10 | Uwekezaji katika amana nyingine | - | - |
| 11 | Mikopo halisi iliyopo | 51,946 | 48,642 |
| 12 | Mali nyingine | 15,528 | 27,099 |
| 13 | Uwekezaji wa hisa | - | - |
| 14 | Akaunti za udhamini | - | - |
| 15 | Mali zisizohamishika, mitambo na vifaa | 3,960 | 4,274 |
| **16** | **JUMLA YA MALI** | **190,896** | **197,207** |
| | **B. DHIMA** | | |
| 17 | Amana za benki nyingine na taasisi za fedha | - | - |
| 18 | Amana za wateja | 96,655 | 110,863 |
| 19 | Dhamana ya malipo kwa fedha taslimu | - | - |
| 20 | Amana maalumu | 6,513 | 5,511 |
| 21 | Maagizo ya malipo/fedha za kuhamisha | - | - |
| 22 | Hundi na hawala za kibenki zilizotolewa | - | - |
| 23 | Limbiko la kodi na gharama zitakazolipwa | 2,631 | 1,081 |
| 24 | Dhima la tozo kwa ajili ya usuluhishi baina ya benki na mteja | - | - |
| 25 | Miamala isiyoshughulikiwa baina ya matawi | - | - |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya kipindi kijacho na tozo nyingine zitakazolipwa baadae | 2,971 | 3,464 |
| 27 | Dhima nyingine | 3,505 | 5,075 |
| 28 | Madeni | 37,052 | 31,000 |
| **29** | **JUMLA YA DHIMA** | **149,327** | **156,994** |
| **30** | **MALI/(DHIMA) HALISI *(16 kutoa 29)*** | **41,569** | **40,213** |
| | **C. FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| 31 | Mtaji wa hisa uliolipwa | 31,420 | 31,420 |
| 32 | Akiba ya mtaji | 29,104 | 29,104 |
| 33 | Mapato yaliyobakizwa | (37,993) | (37,795) |
| 34 | Faida (Hasara) ya kipindi husika | 8,308 | 6,754 |
| 35 | Akaunti nyingine za mtaji | 10,730 | 10,730 |
| 36 | Stahiki ya wenyehisa chache | - | - |
| **37** | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **41,569** | **40,213** |
| 38 | Dhima zisizo dhahiri | 430,854 | 474,451 |
| 39 | Mikopo chechefu | 17,923 | 19,190 |
| 40 | Tengo kwa ajili ya mikopo chechefu | 1,207 | 445 |
| 41 | Mali nyingine chechefu | - | - |
| | **D. BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| (i) | Uwiano wa fedha za wanahisa na jumla ya mali | 22% | 20% |
| (ii) | Uwiano wa mikopo chechefu na jumla ya mikopo ghafi | 33% | 38% |
| (iii) | Uwiano wa mikopo ghafi na jumla ya amana | 52% | 42% |
| (iv) | Uwiano wa mikopo halisi na jumla ya mali halisi | 27% | 25% |
| (v) | Uwiano wa mali zinazozalisha na jumla ya mali | 39% | 31% |
| (vi) | Ongezeko la amana | -11% | 0% |
| (vii) | Ongezeko la mali | -3% | 0% |

### TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO MWAKA ULIOISHIA 30 SEPTEMBA 2024
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo ya Mwaka sasa 30-Sep-24 | Robo ya Mwaka linganishi 30-Jun-24 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 30-Sep-24 | Limbikizo la Mwaka linganishi 30-Sep-23 |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Mapato ya riba | 6,909 | 6,651 | 17,926 | 15,963 |
| 2 | Gharama za riba | (1,907) | (1,456) | (3,212) | (4,231) |
| **3** | **Mapato halisi ya riba (1 kutoa 2)** | **5,003** | **5,195** | **14,714** | **11,732** |
| 4 | Madeni viza yaliyofutwa | - | - | - | - |
| 5 | Punguzo/ongezeko la tengo katika Mikopo | (762) | (724) | (810) | (981) |
| **6** | **Mapato yasiyo ya riba**: | **2,561** | **3,346** | **10,249** | **9,894** |
| | 6.1 Faida /(Hasara) zitokanazo na miamala ya fedha za kigeni | 1,026 | 1,792 | 5,367 | 4,642 |
| | 6.2 Ada na kamisheni | 1,518 | 1,534 | 4,838 | 5,178 |
| | 6.3 Gawio | - | - | - | - |
| | 6.4 Mapato mengine | 17 | 20 | 44 | 74 |
| **7** | **Gharama zisizo za riba:** | **(5,246)** | **(4,603)** | **(14,367)** | **(13,486)** |
| | 7.1 Mishahara na mafao | (2,466) | (1,967) | (6,907) | (6,032) |
| | 7.2 Ada na kamisheni | (408) | (443) | (1,112) | (1,283) |
| | 7.3 Gharama nyingine | (2,373) | (2,193) | (6,372) | (6,171) |
| **8** | **Faida /(Hasara) ya uendeshaji** | **1,555** | **3,214** | **9,763** | **7,159** |
| 9 | Tengo la kodi ya mapato | (1) | (82) | (1,454) | (247) |
| 10 | **Faida / (Hasara) halisi baada ya kodi ya mapato** | **1,554** | **3,132** | **8,308** | **6,912** |
| 11 | **Mapato mengine yaliyojumuishwa (bainisha)** | - | - | - | - |
| **12** | **Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka** | **1,554** | **3,132** | **8,308** | **6,912** |
| 13 | Idadi ya waajiriwa | 137 | 141 | 137 | 141 |
| 14 | Mapato kwa hisa | 247 | 498 | 1,322 | 1,100 |
| **15** | **Idadi ya matawi** | 8 | 8 | 8 | 8 |
| | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | | |
| | (i) Uwiano wa faida kabla ya kodi na wastani wa mali | 3.21% | 4.61% | 5.03% | 5.14% |
| | (ii) Uwiano wa faida baada ya kodi na wastani wa fedha za wanahisa | 15.20% | 40.39% | 20.32% | 44.57% |
| | (iii) Uwiano wa matumizi yasiyo ya riba na mapato ghafi | 55.40% | 46.04% | 50.99% | 52.16% |
| | (iv) Uwiano wa mapato halisi ya riba na wastani wa mali zinazozalisha | 11.89% | 8.24% | 8.74% | 9.31% |

| | ***Jina na Cheo*** | ***Saini*** | ***Tarehe*** |
|---|---|---|---|
| 1 | Gbenga Makinde<br>**Mkurugenzi Mtendaji** | ***Imesainiwa*** | *28 Oktoba 2024* |
| 2 | Fina Andrew<br>**Kaimu Afisa Mkuu wa Fedha** | ***Imesainiwa*** | *28 Oktoba 2024* |
| 3 | Joseph Ringa<br>**Mkaguzi Mkuu wa Ndani** | ***Imesainiwa*** | *28 Oktoba 2024* |

Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi, tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006, na zinaonesha hali halisi.

| | ***Jina na Cheo*** | ***Saini*** | ***Tarehe*** |
|---|---|---|---|
| 1 | Amb.Tuvako Manongi<br>**Mkurugenzi** | ***Imesainiwa*** | *28 Oktoba 2024* |
| 2 | Ebele Ogbue<br>**Mkurugenzi** | ***Imesainiwa*** | *28 Oktoba 2024* |

### TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO/MWAKA ULIOISHIA 30 SEPTEMBA 2024
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | Robo ya Mwaka ya sasa 30-Sep-24 | Robo ya Mwaka linganishi 30-Jun-24 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 30-Sep-24 | Limbikizo la Mwaka linganishi 30-Sep-23 |
|---|---|---|---|---|
| **I: Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | | | |
| Mapato/(Hasara) Halisi | **1,554** | **3,339** | **8,308** | **6,912** |
| Marekebisho kwa Ajili ya: | | - | - | - |
| - Hasara Katika Mali | 1,074 | 241 | 1,314 | 1,888 |
| - Badiliko Halisi Katika Mikopo | (3,304) | 1,059 | (2,245) | (1,465) |
| - Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | - | - | - | - |
| - Mabadiliko Halisi Katika Amana | (13,207) | (45,921) | (59,128) | (26,302) |
| - Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi Zilizoafikiwa | (44) | (1,626) | (1,669) | (2,125) |
| - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | 665 | (17,397) | (16,732) | 2,074 |
| -Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | 11,571 | 25,214 | 36,785 | 19,276 |
| - Kodi Iliyolipwa | (1) | (1,287) | (1,288) | (165) |
| -Mengineyo (bainisha) | - | - | - | - |
| *Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji* | **(1,692)** | **(36,378)** | **(34,655)** | **(86)** |
| **II. Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | | | | |
| Gawio Lililopokewa | - | - | - | - |
| Ununuzi wa Mali za Kudumu | (68) | (94) | (162) | (2,810) |
| Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | - | - | - | - |
| Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| Mengineyo (bainisha) | - | - | - | - |
| *Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji* | **(68)** | **(94)** | **(162)** | **(2,810)** |
| ***III. Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha:*** | | | | |
| Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | - | - | - |
| Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | - | - | - | - |
| Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | 6,052 | 31,000 | 37,052 | - |
| Mengineyo (bainisha) | - | - | - | - |
| ***Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Kifedha*** | **6,052** | **31,000** | **37,052** | **-** |
| IV. Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu: | | | | |
| Ongezeko / Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu | **4,291** | **(5,471)** | **(1,180)** | **(4,033)** |
| Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo Mwaka | 18,890 | 24,362 | 24,362 | 45,137 |
| Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo Mwaka | **23,181** | **18,890** | **23,181** | **41,104** |

### TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 30 SEPTEMBA 2024
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato yaliyobakizwa | Ziada ya Kisheria | Tengo la ziada ya jumla | Mengineyo | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mwaka wa sasa 2024** | | | | | | | |
| Salio la mwanzo wa mwaka | 31,420 | 29,104 | (37,795) | 10,730 | - | - | 33,459 |
| Faida/(Hasara) Halisi baada ya kodi ya mapato | - | - | 8,308 | - | - | - | 8,308 |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya kisheria | - | - | - | - | - | - | - |
| Tengo la ziada ya jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | (198) | - | - | - | (198) |
| Share issued | | | - | | - | | |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **31,420** | **29,104** | **(29,685)** | **10,730** | **-** | **-** | **41,569** |
| **Mwaka uliopita 2023** | | | | | | | |
| Salio la mwanzo wa mwaka | 31,420 | 29,104 | (39,925) | 5,097 | - | - | 25,696 |
| Faida/(Hasara) Halisi baada ya kodi ya mapato | - | - | 7,763 | - | - | - | 7,763 |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya kisheria | - | - | (5,633) | 5,633 | - | - | - |
| Tengo la ziada ya jumla | - | - | - | - | | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| Share issued | | | | | - | | |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **31,420** | **29,104** | **(37,795)** | **10,730** | **-** | **-** | **33,459** |

**United bank of Africa (T) Ltd** ni benki ya kiafrika inayoongoza Afrika kwa kutoa huduma za kibenki kwa wateja zaidi ya milioni 13 katika matawi zaidi ya 1000 barani Afrika, Marekani, Ulaya na Umoja wa Nchi za Kiarabu.

**Afrika Mashariki na Kusini** | **Afrika ya Kati** | **Afrika Magharibi** | **Ulaya** | **Marekani** | **Umoja wa Nchi za Kiarabu**

- Tanzania
- Kenya
- Congo DRC
- Mozambique
- Uganda
- Zambia
- Cameroon
- Gabon
- Tchad
- Congo Brazzaville
- Ghana
- Benin
- Burkina Faso
- Cote D'Ivore (CDI)
- Liberia
- Sierra Leone
- Senegal
- Mali
- Guinea
- UK
- France
- New York
- Dubai

30C/30D Barabara ya Nyerere, S.L.P 80514, Dar es Salaam, Tanzania. Simu: +255 789 784 302 | Barua Pepe: customerservicetz@ubagroup.com

ubatanzania

# NAMUNGO YAAHIDI USHINDI KWA MASHABIKI NYUMBANI

**Na Somoe Ng'itu**

BAADA ya kupata ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Pamba Jiji FC, nahodha wa Namungo, Jacob Massawe, amesema wanaahidi kuendeleza furaha kwa mashabiki wao katika mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara zinazoendelea.

Ushindi wa juzi umewafanya Namungo waliokuwa nyumbani kwao kwenye Uwanja wa Majaliwa kufikisha pointi tisa baada ya kucheza michezo tisa, wakipanda hadi nafasi ya 11 katika msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Akizungumza na gazeti hili baada ya mechi, Massawe alisema ligi imekuwa na ushindani, lakini watahakikisha hawapotezi pointi wanapocheza kwenye uwanja wa nyumbani.

> **Massawe alisema wachezaji wa timu hiyo wanaendelea kujiimarisha na kufuata vizuri maelekezo ya benchi la ufundi katika kila mechi, lakini wakati mwingine bahati inakuwa upande wa wapinzani wao.**

"Tunamshukuru Mungu tumepata ushindi, malengo yetu ni kuendelea kupambana ili kutopoteza pointi, tunataka kuwapa furaha mashabiki wetu hasa tunapocheza nyumbani, lakini wafahamu hakuna mechi rahisi, ushindani katika ligi unazidi kuwa mkubwa, hii inasababisha kila mechi kuwa sawa na fainali," Massawe alisema.

Naye Kocha Msaidizi wa timu hiyo, Ngawina Ngawina, alisema wanaendelea kufanyia kazi makosa ili kuhakikisha wanafanya vizuri katika kila mechi iliyoko mbele yao.

Ngawina alisema kupoteza umakini kwa baadhi ya wachezaji wao kunasababisha kuifanya mechi inakuwa ngumu.

"Pia tumekuwa hatutumii vizuri nafasi za kufunga mabao tunazotengeneza, hata hivyo tunarudi katika uwanja wa mazoezi kulifanyia kazi tatizo hili, tunaahidi kila mechi tutacheza tofauti kulingana na aina ya mpinzani tunayekutana naye," alisema kocha huyo.

Kikosi cha Namungo kinatarajia kusafiri kwenda Dar es Salaam kuwafuata KMC kwa ajili ya mechi nyingine ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayochezwa kesho kwenye Uwanja wa KMC Complex, huku ikisubiri kupangiwa siku nyingine ya mchezo wao dhidi ya JKT Tanzania ambao ulitarajiwa kufanyika Novemba 4, mwaka huu, baada ya kikosi cha Maafande hao kupata ajali walipokuwa njiani kutoka jijini Dodoma mapema wiki hii.

Ligi Kuu Tanzania Bara inatarajiwa kuendelea tena leo kwa vinara Singida Black Stars kuwakaribisha mabingwa watetezi, Yanga kwenye Uwanja wa New Amaan Complex ulioko Zanzibar.

**MAGONGO...**



Watoto wakicheza mpira wa magongo katika Uwanja wa Jakaya Kikwete jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# *Kuiona Taifa Stars, Sudan bure*

**Na Somoe Ng'itu**

SHIRIKISHO la Soka Tanzania (TFF), limetangaza kuwa mashabiki wataingia bure kushuhudia mechi ya marudiano kati ya Timu ya Taifa (Taifa Stars), dhidi ya Sudan itakayochezwa Jumapili kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Katika mechi ya kwanza iliyochezwa nchini Mauritania, wenyeji Sudan walipata ushindi wa bao 1-0.

Taifa Stars na Sudan zinakutana katika mechi ya kusaka tiketi ya kufuzu kucheza fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN), ambazo zitafanyika mwakani hapa nchini.

Ofisa Habari na Mawasiliano wa TFF, Clifford Ndimbo, alisema jana kuwa lengo la kutoweka kiingilio ni kutaka kutoa nafasi kwa mashabiki wengi kujitokeza katika mchezo huo ili kuwaongezea hamasa wachezaji.

Ndimbo alisema kikosi cha timu hiyo kinachoongozwa na Kocha Mkuu, Bakari Shime, kinaendelea vema na maandalizi ya mechi hiyo ya marudiano ambapo juzi jioni wachezaji walifanya mazoezi kwenye Kituo cha Ufundi cha Dakar, Senegal.

"Tunapenda kuwatangazia mashabiki wa soka walioko Dar es Salaam na mikoa ya jirani kujitokeza kwa wingi kuja kuwasapoti wachezaji wetu, hii ni mechi muhimu sana, tunaamini itawapa nguvu ya kupambana," alisema Ndimbo.

Hata hivyo, Taifa Stars, Kenya (Harambee Stars) na Uganda wameshakata tiketi ya kushiriki fainali hizo kwa sababu wao ni wenyeji.

# Simba Queens kamili kuifuata Ceasiaa Iringa

**Na Mwandishi Wetu**

UONGOZI wa Simba Queens umesema timu yao itaondoka mapema kuelekea Iringa kwa ajili ya mechi ya Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania (TWPL), dhidi ya Ceasiaa itakayochezwa Novemba 5, mwaka huu kwenye Uwanja wa Samora mkoani humo.

Meneja wa Simba Queens, Selemani Makanya, aliliambia gazeti hili jana kuwa kikosi chao kinaendelea vema na mazoezi na wamepanga kuondoka mapema Dar es Salaam ili kwenda kuzoea hali ya hewa ya Iringa.

Makanya alisema wanafahamu mechi hiyo haitakuwa rahisi kwa kila upande kwa sababu timu zote zina wachezaji wenye uzoefu na ligi hiyo.

Meneja huyo alisema Simba Queens imejiimarisha na kwao kila mechi ni sawa na fainali na hawatadharau wapinzani wao.

"Kikosi chetu kimekuwa na mazoezi kwa muda wote wa mapumziko ya ligi, lengo ni kujiimarisha katika kila idara, tunajua hakuna mechi rahisi, kila mechi ni sawa na fainali, tunataka kwenda kuchukua pointi tatu Iringa na kuendelea kujiimarisha katika msimamo wa ligi," alisema Makanya.

Aliongeza kuwa kipa wao chaguo la kwanza, Caroline Rufa, ambaye alikuwa majeruhi, hali yake inaridhisha.

Naye Kocha Msaidizi wa timu hiyo, Mussa Hassan 'Mgosi', aliliambia gazeti hili ligi ya msimu huu ni ngumu na hiyo inatokana na timu zote kufanya usajili mzuri.

Mgosi alisema wamejiandaa kuonesha kiwango bora katika kila mechi kwa sababu malengo yao ni kutetea ubingwa wa ligi.

"Tunahitaji kurudi tena katika mashindano ya CECAFA (Afrika Mashariki na Kati), ni lazima tuwe mabingwa, tunataka kurekebisha tulipokosea ili msimu ujao tukafanye vizuri katika michuano hiyo ya kimataifa," Mgosi alisema.

Mechi nyingine za Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania zitakazochezwa Novemba 5, mwaka huu, ni kati ya Yanga Princess na Mashujaa Queens wakati JKT Queens itawaalika Mlandizi Queens huku Bunda Queens ikiifuata Gets Program na Fountain Gate Girls ikiwaalika Alliance Girls.



Simba Queens yenye pointi sita ndio vinara wa Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania inayojumuisha timu 10 kutoka mikoa mbalimbali.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### AMORIN AKUBALI KUINOA UTD

KOCHA wa Sporting, Ruben Amorim, amekubali kuwa kocha ajaye wa Manchester United kutokana na kufukuzwa kwa Erik ten Hag juzi, Jumatatu. ***(Manchester Evening News)***

### TERZIC AWANIWA DORTMUND

KOCHA wa zamani wa Borussia Dortmund, Edin Terzic, ndiye anayelengwa na Manchester United, baada ya Thomas Tuchel kuteuliwa kuwa kocha wa England. ***(Sun)***

### MBEUMO AWINDWA ARSENAL

ARSENAL wanatathmini dau la kutaka kumsajili mshambuliaji wa Brentford raia wa Cameroon, Bryan Mbeumo, mwenye umri wa miaka 25. ***(Football Insider)***

### MURILLO ATAJWA LIVERPOOL

LIVERPOOL inafikiria kumnunua beki wa kati wa Nottingham Forest na Brazil, Murillo mwenye umri wa miaka 22, lakini wanaweza kukabiliwa na ushindani kutoka kwa Chelsea. ***(TeamTalks)***

### FRANK PIA AFIKIRIWA UNITED

KOCHA wa Brentford, Thomas Frank, ni miongoni mwa makocha ambao Manchester United wanafikiria kuwachukua kwa nafasi ya Erik Ten Hag. ***(ESPN)***

### ISAK KUSHINIKIZA KUONDOKA

MSHAMBULIAJI wa Sweden, Alexander Isak mwenye umri wa miaka 25, anaweza kushinikiza kuondoka Newcastle United katika dirisha dogo la usajili la majira ya joto. ***(Football Insider)***

### KOKCU AFUATILIWA LIVER

LIVERPOOL wanamfuatilia kiungo wa kati wa Benfica na Uturuki, Orkun Kokcu, 23. ***(Football Insider)***

### JESUS AKATALIWA ARSENAL

ARSENAL wamekataa mpango wa Palmeiras kutaka kumsajili mshambuliaji wa Brazil, Gabriel Jesus, 27. ***(ESPN)***

### QUENDA ATAKIWA UNITED

KLABU ya Manchester United wanavutiwa na kiungo wa kati wa Sporting, Mreno mwenye umri wa miaka 17, Geovany Quenda. ***(A Bola)***

### WOOD MKATABA MPYA

KLABU ya Nottingham Forest imeanza mazungumzo na mshambuliaji wa New Zealand, Chris Wood mwenye umri wa miaka 32, kuhusu mkataba mpya. ***(Telegraph)***

### BETO KUONDOKA EVERTON

MSHAMBULIAJI wa Guinea-Bissau, Beto mwenye umri wa miaka 26, anafikiria kuondoka Everton ili kutafuta nafasi ya kuchezea kikosi cha kwanza. ***(Football Insider)***

## DONDOO … KA MAGAZET… AYA



# RODRI NDIYE MSHINDI WA BALLON D'OR 2024

**PARIS,** Ufaransa

KIUNGO wa kati wa Manchester City na Hispania, Rodri, ametangazwa kuwa mshindi wa Tuzo ya Ballon d'Or katika hafla iliyofanyika usiku wa kuamkia jana jijini Paris, Ufaransa.

**Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28, ambaye alipoteza mchezo mmoja pekee msimu uliopita kwa klabu na taifa, alitunukiwa tuzo hiyo jijini Paris baada ya kuisaidia Hispania kushinda Euro 2024 Julai mwaka huu.**

Pia alishinda Ligi Kuu England, Uefa Super Cup na Klabu Bingwa ya Dunia akiwa na Man City. Rodri, mchezaji wa kwanza katika historia ya klabu hiyo kushinda Ballon d'Or, alishinda tuzo hiyo mbele ya winga wa Real Madrid na Brazil, Vinicius Jr.

Kiungo wa kati wa Real Madrid, Jude Bellingham, alikuwa wa tatu - akiwa mchezaji wa juu zaidi wa England aliyemaliza katika tuzo hiyo tangu Frank Lampard kumaliza katika nafasi ya pili mwaka 2005.

Real Madrid ilishinda tuzo ya klabu bora ya mwaka na kocha Carlo Ancelotti alitangazwa kuwa mshindi wa tuzo ya kocha bora wa mwaka, lakini hakukuwa na yeyote kutoka klabu hiyo aliyehudhuria kupokea zawadi hizo.

Iliripotiwa mapema Jumatatu kuwa Real Madrid walikuwa wakisusia sherehe hizo baada ya ripoti kuwa Vinicius angeshinda Ballon d'Or.

"Ni siku maalum kwangu, familia yangu na nchi yangu," alisema Rodri, ambaye alionekana jukwaani akitembea kwa magongo baada ya kupasuka mishipa yake ya goti Septemba mwaka huu.

"Leo si ushindi kwangu, ni kwa mpira wa miguu wa Hispania kwa wachezaji wengi ambao hawajashinda na wamestahili, kama Andres Iniesta, Xavi Hernandez, Iker Casillas, Sergio Busquets na wengine wengi. Ni kwa ajili ya soka la Hispania na sura ya kiungo cha kati."

Tuzo ya Ballon d'Or inamtambua mwanasoka bora wa mwaka na hupigiwa kura na baraza la waandishi wa habari kutoka kila moja ya nchi 100 bora katika viwango vya ubora vya Fifa duniani kwa wanaume.

## ●●● Martinez kipa bora huku Kane, Mbappe na Yamal nao wakibeba tuzo za...

#### Kane, Mbappe washinda tuzo ya Gerd Muller

Harry Kane na Kylian Mbappe walishinda kwa pamoja tuzo ya Gerd Muller - tuzo ya mfungaji bora - baada ya wote kufunga mabao 52 katika mashindano yote msimu uliopita.

Huku fowadi wa Real Madrid na Ufaransa Mbappe akiwa hayupo, nahodha wa England Kane alikabidhiwa tuzo hiyo peke yake kutokana na msimu mzuri wa kwanza akiwa na Bayern Munich.

#### Yamal ashinda tuzo ya Kopa

Tuzo ya Kopa Trophy, iliyotolewa kwa mchezaji aliyefanya vizuri zaidi mwenye umri chini ya miaka 21, ilienda kwa winga wa Barcelona na Hispania, Lamine Yamal.

Yamal, ambaye alitimiza umri wa miaka 17 Julai, aliichezea Barcelona mechi 50 msimu uliopita, akifunga mabao saba na asisti saba.

Mlinda mlango wa Aston Villa na Argentina, Emiliano Martinez alishinda taji la Yashin Trophy - tuzo ya golikipa bora - kwa mwaka wa pili mfululizo.

# AMORIM AONGOZA KUWANIA UKOCHA MANCHESTER UTD




**MANCHESTER,** England

RUBEN Amorim ameibuka kuwa mgombea anayeongoza kuchukua mikoba ya Erik ten Hag katika Klabu ya Manchester United, chanzo kiliiambia ESPN.

Kocha huyo wa Sporting CP, anafahamu nia hiyo, huku United ikijaribu kufanya haraka kutaja kocha mpya wa kudumu baada ya kumteua Ruud van Nistelrooy ambaye atahudumu kwa muda. Ten Hag alifutwa kazi Jumatatu baada ya kichapo cha mabao 2-1 kutoka kwa West Ham United Jumapili.

United italazimika kulipa ada ya karibu pauni milioni 10 kumchukua Amorim ili avunje mkataba wake na Sporting Lisbon, chanzo kiliiambia ESPN. Chanzo hicho kiliongeza kuwa United pia wameuliza kuhusu kupatikana kwa Kocha wa Brentford, Thomas Frank.

Kifungu cha kutolewa kwa Frank katika Uwanja wa Gtech Community ni karibu mara mbili ya kile cha Amorim. Amorim alikuwa akihusishwa na kazi ya Liverpool kabla ya Arne Slot kumrithi Jurgen Klopp majira ya joto na kufanya mazungumzo na West Ham kabla ya kumteua Julen Lopetegui.

Mchezaji huyo wa zamani wa Kimataifa wa Ureno mwenye umri wa miaka 39, amekuwa akiinoa Sporting Lisbon tangu 2020. Alishinda taji la Ureno mwaka 2021 na 2024 licha ya ushindani mkali kutoka kwa FC Porto na Benfica.

Amorim pia amehusishwa na Manchester City baada ya Mkurugenzi wa Soka wa Sporting Lisbon, Hugo Viana, kukubali kumrithi City, Txiki Begiristain, kwenye Uwanja wa Etihad mwishoni mwa msimu. Akizungumza juzi, Jumatatu, Amorim alisitasita kuhusu uhusiano na kazi ya United.

"Nilikuwa tayari nikitarajia swali hili na ni wazi sitazungumza juu ya siku zijazo, kwa sababu vinginevyo nitalazimika kutoa maoni," alisema.

"Ninajivunia kuwa kocha wa Sporting, ni hivyo tu."

Frank pia alifanya mkutano na wanahabari siku hiyo na pia hakuzungumza kuhusu nia hiyo kutoka Old Trafford.

"Ni swali nyeti sana," alisema Frank. "Nina jukumu kwa Brentford, klabu na mashabiki. Nimesema mara nyingi, mara nyingi nina furaha sana hapa; nadhani ni moja ya klabu bora zaidi duniani."

## Balotelli arejea Serie A

**ROME,** Italia

MSHAMBULIAJI wa zamani wa Italia, Mario Balotelli, amejiunga na Klabu ya Genoa inayoshiriki Ligi Kuu Italia, Serie A, kama mchezaji huru.

Balotelli mwenye umri wa miaka 34, alifanyiwa uchunguzi wa kimatibabu Jumatatu kabla ya kusaini mkataba na Genoa kwa muda uliosalia wa msimu.

"Nimesukumwa. Sitaki kuzungumza mengi. Nataka tu kuanza," alisema Balotelli.

"Nitajitolea," aliongeza, akiwahutubia mashabiki.

Mchezaji huyo wa zamani wa Manchester City alikuwa hana timu tangu alipoondoka Klabu ya Adana Demirspor ya Uturuki Juni mwaka huu.

Alishiriki mara ya mwisho katika Ligi Kuu Italia msimu wa 2019-2020 akiwa na Brescia, ingawa alicheza Serie B katika Klabu ya Monza katika kampeni ya 2020-21.

Genoa wamemgeukia Balotelli kwa kuwa wanasumbuliwa na majeraha. Kikosi cha Alberto Gilardino kina wachezaji saba ambao hawapatikani, wakiwamo mshambuliaji Vitinha, Junior Messias na Caleb Ekuban.

"Balotelli? Hadithi yake inazungumza kwa niaba yake, lakini hawezi kutatua matatizo ya Genoa peke yake," alisema Gilardino baada ya kushindwa kwa mabao 3-0 Jumapili na Lazio hivyo kuiacha klabu hiyo katika nafasi ya 18 kwenye Serie A.

"Ni kawaida kwamba akifika na moto kwenye timu anaweza kuwa na thamani kwa ubora wake wa kiufundi, anaweza kutupa utu."

Balotelli, ambaye alifunga mabao saba katika mechi 16 za ligi msimu uliopita, alikuwa akifanya mazoezi peke yake huko Brescia huku akitathmini ofa.

Genoa wameshinda mchezo mmoja na kupoteza mechi tano kati ya tisa za ligi msimu huu kuelekea mchezo wa nyumbani wa Alhamisi dhidi ya Fiorentina.

# *Alexander-Arnold atajiunga Real Madrid - Carragher*

**LIVERPOOL,** England

MLINZI wa zamani wa Liverpool, Jamie Carragher ana wasiwasi kwamba nia ya Trent Alexander-Arnold, kutwaa tuzo ya Ballon d'Or itamfanya aondoke katika klabu hiyo na kujiunga na Real Madrid.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26, mkataba wake unamalizika mwishoni mwa msimu huu, pamoja na wachezaji wenzake Mohamed Salah na Virgil van Dijk, na hakuna dalili kwamba beki huyo wa pembeni anakaribia kusaini mkataba mpya.

Badala yake, Alexander-Arnold amekuwa akihusishwa na kuhamia kwa mabingwa mara 15 wa Ligi ya Mabingwa Ulaya, Real Madrid, ambao kwa kushangaza walichapwa mabao 4-0 na wapinzani wao, Barcelona wakiwa nyumbani wikendi hii iliyopita kwenye Clasico ya kwanza ya msimu huu.

PSG pia wametajwa kumtaka Alexander-Arnold, ambaye alifichua kabla ya Liverpool kutoka sare ya mabao 2-2 na Arsenal kwamba anataka kuwa beki wa kwanza wa pembeni kuwahi kushinda Ballon d'Or inayotamaniwa sana.

Alexander-Arnold alikiri kwamba anataka kutengeneza historia na kukumbukwa kama "beki wa kulia bora zaidi kuwahi kucheza soka" - kitu ambacho Carragher anahisi atakifanikisha iwapo tu ataishia kuondoka Liverpool na kwenda Madrid.

"Wazo langu la kwanza nilipoona kwamba hutashinda Ballon d'Or kama beki wa kulia wa Liverpool," alisema Carragher akiiambia Sky Sports.

"Washindi wa Ballon d'Or kwa kawaida huchezea Real Madrid au Barcelona. Hapo ndipo wachezaji bora zaidi duniani.

"Ikiwa hiyo ndiyo dhamira yake kuu - nadhani aliulizwa kuhusu kushinda Ligi ya Mabingwa, Kombe la Dunia au Ballon d'Or na akaenda kushinda Ballon d'Or - ambayo nadhani ni ya kushangaza au ya ajabu kwa sababu mchezo wa timu, lakini ana malengo makubwa na kwa nini usiwe na kazi moja tu, yeye ni beki wa pembeni wa kipekee na anashangaza kabisa."

# MASHINDANO BAISKELI SHINYANGA SASA YANUKIA KUWA YA KIMATAIFA

**Na Mwandishi Wetu**

BAADA ya kufanyika kwa mafanikio kwa misimu mitano sasa, Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Anamringi Macha, ameishauri Benki ya CRDB kuyapandisha hadhi mashindano ya Baiskeli Shinyanga kuwa ya kimataifa.

**Macha alitoa ushauri huo kwenye mashindano ya mbio hizo yaliyofanyika mwishoni mwa wiki yakijumuisha wakimbiaji kutoka mikoa yote ya Kanda ya Ziwa na maeneo mengine nchini.**

"Mbio hizi za baiskeli ni utambulisho wa mkoa wetu kwani leo taifa zima linatambua kuna jambo linaendelea hapa Shinyanga. Nafurahi kuona idadi kubwa ya wananchi mmejitokeza kushiriki, hivyo kupata nafasi ya kufahamiana na kujumuika pamoja kwa furaha. Ninachowaomba waandaaji ambao ni Benki ya CRDB, wakaribisheni washiriki kutoka nje ya mipaka ya Tanzania. Nafahamu mnatoa huduma Burundi na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), waleteni waendesha baiskeli kutoka huko waje tushindane nao.

"Shinyanga tupo tayari kushindanishwa na yeyote yule, hivyo hata kama mtaona kuna waendesha baiskeli katika nchi nyingine za Afrika Mashariki, wakaribisheni waje tuoneshane umwamba. Naamini kabisa, zawadi zote wataziacha hapa na wataenda kusimulia walichokiona Shinyanga," alisema mkuu huyo wa mkoa.

Licha ya washindi kupewa zawadi, mbio hizo zilitanguliwa na uchangiaji wa damu ambapo zaidi ya chupa 500 zilipatikana suala ambalo Kaimu Meneja wa Kanda ya Ziwa wa Benki ya CRDB, Anselm Mwenda, aliwashukuru wafanyakazi wenzake pamoja na wananchi wote walioshiriki kuchangia akisema zitakuwa na manufaa makubwa kwa wagonjwa wenye uhitaji.

"Zaidi ya chupa 507 za damu salama zilizokusanywa si haba, zitasaidia kukidhi mahitaji kwa baadhi ya wagonjwa. Napenda kutumia fursa hii pia kuwakumbusha wananchi umuhimu wa kuchangia damu kwani hujui itamsaidia nani kuokoa maisha yake. Kila siku tunasikia ajali na wagonjwa wakikimbizwa hospitalini, miongoni mwao wapo waliopungukiwa damu hivyo tujitahidi kujitoa kwa ajili yao," alisema Mwenda akibainisha kuwa mwaka huu kimepatikana kiasi kingi zaidi ikilinganishwa na misimu iliyopita.

Kuhusu wito wa kuyafanya Mashindano ya Baiskeli Shinyanga kuwa ya kimataifa, Mwenda alisema watalifanyia kazi kwa kuwasiliana na mamlaka husika kuona waanzie wapi kuwapata washiriki kutoka mataifa ya Afrika Mashariki.

"Tumeupokea ushauri wa mheshimiwa mkuu wa mkoa. Tutaufanyia kazi ndani, kisha tutazishirikisha mamlaka husika kuona namna ya kuileta jamii ya Afrika Mashariki hapa Shinyanga. Ni jambo linalowezekana, naamini mwakani mashindano haya yanaweza kuwa na sura ya kimataifa," alisema Mwenda.

Katika mashindano hayo, wanaume walikimbia umbali wa kilomita 150 na washindi walikuwa Boniface Ngwata kutoka Mwanza, Masunga Duba wa Simiyu na Frank Emmanuel kutoka jijini Dar es Salaam. Katika kundi hili, mshindi wa kwanza alijinyakulia Sh. milioni 1.5, wa pili aliondoka na Sh. 800,000 na wa tatu alijinyakulia Sh. 400,000.

Kundi la pili lilikuwa la wakimbiaji chipukizi waliokimbia kilomita 80 ambalo Frank George wa Shinyanga aliongoza akifuatiwa na Joseph Paschal na Emmanuel George wote wa Shinyanga. Washindi hawa waliondoka na Sh. 800,000 kwa mshindi wa kwanza huku wa pili akizawadiwa Sh. 600,000 na wa tatu Sh. 300,000.

Kundi la mwisho lilikuwa la wanawake ambao walishindana kukamilisha mizunguko 20 katika uwanja wa mpira na zawadi zao zilikuwa Sh. 500,000 kwa mshindi wa kwanza, Sh. 300,000 na Sh. 200,000 kwa msindi wa pili na wa tatu. Kundi hili liliongozwa na Makirikiri Joseph wa Shinyanga alikifuatiwa na Florah Samwel wa Dar es Salaam na Sindano Makirikiri wa Shinyanga pia. Mshindi wa nne katika makundi yote aliondoka na Sh. 100,000 na wale walioshika nafasi ya tano mpaka ya 10 walizawadiwa Sh. 50,000 kila mmoja.

## PAMBA MECHI 10 BILA USHINDI

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA mkongwe nchini, Juma Mgunda, ameanza na mguu mzuri kwenye kikosi cha Namungo kwa kupata ushindi wa kwanza tangu alipochukua mikoba ya kuifundisha timu hiyo huku akiiongezea Pamba Jiji FC rekodi yao mbaya ya kutoshinda kufikia mechi 10 hadi sasa msimu huu.

Katika mchezo huo uliopigwa juzi usiku kwenye Uwanja wa Majaliwa, Ruangwa mkoani Lindi na Namungo kushinda 1-0, bao hilo pekee lilifungwa na Ibrahim Mkoko dakika ya 12, na kuifanya timu hiyo kupata ushindi wa kwanza baada ya kupoteza mitatu mfululizo.

Mara ya mwisho kushinda ilikuwa ni Septemba 28, ilipoifunga Prisons bao 1-0, baada ya hapo ilichapwa 1-0 dhidi ya Azam, ikazabwa mabao 2-0 dhidi ya Singida Black Stars, kabla ya kukutana na kipigo cha mabao 3-0 dhidi ya Simba Ijumaa iliyopita.

Wakati ikisulubiwa na Simba kwenye Uwanja wa KMC, Mwenge, Dar es Salaam, Mgunda alikuwa amekaa jukwaani akishuhudia kwani ilikuwa ni siku moja tu tangu atangazwe kujiunga nayo.

Ushindi huo unaisogeza juu kidogo timu hiyo hadi nafasi ya 11, ikifikisha pointi tisa, ikicheza michezo tisa, ikishinda mitatu na kupoteza sita, ikiwa haijatoka sare hata mchezo mmoja.

Namungo na Yanga ndizo timu pekee kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara hazijaonja ladha ya sare.

Kipigo cha bao 1-0 ilichokipata Pamba Jiji kinaendeleza mlolongo wa matokeo mabovu ya timu hiyo tangu ilipopanda daraja msimu huu.

Ikiwa imeshacheza michezo 10, haijashinda hata mchezo mmoja ikiwa ni timu pekee ambayo haijaonja utamu wa ushindi kwenye Ligi Kuu, ikipoteza michezo mitano na sare tano.

Inakamata nafasi ya 15 kwenye msimamo wa Ligi Kuu wenye timu 16, ikiwa ina pointi tano tu mpaka sasa, ikiizidi KenGold inayoburuza mkia ikiwa na pointi moja tu mkononi hadi sasa.

## Yanga, Singida BS vita vya kileleni leo

INATOKA UKURASA 24

pointi 24 na kuiacha Singida ikibaki na pointi 22.

Iwapo Singida itashinda mchezo wa leo, itazidi kujichimbia kileleni na kufikisha pointi 25, huku Yanga ikisalia na pointi zake 21 ilizonazo.

Sare yoyote kwa timu hizo mbili itakuwa nafuu kwa Singida kwani itakuwa na pointi 23, Yanga ikifikisha pointi 22, ingawa mabingwa watetezi hao watakuwa bado na mchezo mmoja mkononi.



Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Anamringi Macha (aliyevaa jaketi kushoto), akiwa pamoja na washindi wa msimu wa tano wa Mbio za Baiskeli Shinyanga zinazoandaliwa na Benki ya CRDB zikilenga kumwenzi Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, pamoja na kuchangia damu kwa wagonjwa wenye uhitaji. **MPIGAPICHA WETU**

## *Simba nguvu zote sasa kwa Mashujaa*

INATOKA UKURASA 24

wamecheza mechi nyingi mfululizo wakipumzika kwa saa chache," alisema Fadlu.

Meneja Habari na Mawasiliano wa klabu hiyo, Ahmed Ally, amesema pointi tatu ambazo walitegemea kuzipata kwa JKT Tanzania, sasa watakwenda kuzichukua kwa Mashujaa FC mkoani Kigoma.

"Tupo kwenye maandalizi makali, na tunafanya maandalizi ya safari ili kuelekea mjini Kigoma kucheza na Mashujaa, kwa hiyo nawaambia wanachama na mashabiki wote wa Simba, baada ya kuahirishwa mchezo wetu dhidi ya JKT Tanzania, nguvu zote sasa tunaelekeza Kigoma dhidi ya Mashujaa Novemba Mosi. Furaha yetu imesogezwa mbele, tukutane Kigoma tukafurahi tena," alisema Ahmed.

Ratiba inaonesha kuwa baada ya mchezo huo wa Ijumaa, Simba itashuka tena dimbani Novemba 5, mwaka huu katika Uwanja wa KMC, Mwenge, Dar es Salaam kucheza dhidi ya KMC FC, ambapo 'Wekundu wa Msimbazi' hao ndiyo watakuwa wenyeji kikanuni, kabla ya mapumziko ya Kalenda ya FIFA.

Baada ya kalenda hiyo, Simba na itarejea tena dimbani, Novemba 21, kucheza dhidi ya Pamba Jiji, Uwanja wa CCM Kirumba, Mwanza, ikiwa ni mchezo wa mwisho, kabla ya kuanza mechi za kimataifa kwa mchezo wa kwanza, Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya Bravos do Maquis, Novemba 28, na kurejea tena Ligi Kuu Desemba Mosi, mwaka huu, kucheza dhidi ya Singida Black Stars.

# Michezo

Jumatano Oktoba 30, 2024

Nipashe




Balotelli arejea Serie A UKURASA 22

BALLON D'OR...



Kiungo wa Kati wa Manchester City na Hispania, Rodri, akiwa katika picha tofauti. Katikati akiwa na Tuzo ya Ballon d'Or baada ya kutangazwa mshindi juzi nchini Ufaransa, na kushoto akiwa na Kombe la Euro 2024 Julai mwaka huu alipoiwezesha Hispania kulibeba wakati kulia akishangilia baada ya kuihakikishia Man City ubingwa wa Ligi Kuu England msimu uliopita. **HABARI UK. 21. PICHA: MTANDAO**

# YANGA SC, SINGIDA BS VITA VYA KILELENI LEO

**Na Adam Fungamwango**

●●● Zinashuka dimbani Zanzibar kila moja ikipania kuondoka na alama tatu, makocha...

KOCHA Mkuu wa Yanga, Miguel Gamondi, amesema mchezo wa leo dhidi ya Singida Black Stars ni kama wa fainali kwani iwapo watapata pointi tatu watakwenda kukaa kwenye kilele cha msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

**Mchezo kati ya timu hizo mbili, Mabingwa Watetezi wa Ligi Kuu na vinara wa msimamo wa ligi unapigwa leo usiku saa 2:30 usiku, Uwanja wa New Amaan Zanzibar, huku Singida Black Stars ikihitaji matokeo mawili, ushindi au sare ili kuweza kuendelea kutesa juu ya msimamo.**

Kocha huyo amesema anatarajia timu yake kucheza kwenye staili yake iliyozoeleka kutokana na mazingira ya uwanja kuruhusu, ingawa akiiheshimu Singida Black Stars kuwa ni timu imara yenye wachezaji wenye ubora mkubwa na wazoefu.

"Ni mechi nzuri kama ya fainali, iwapo tutashinda tutakwenda kukaa kileleni mwa msimamo wa ligi kitu ambacho ni moja kati ya malengo yetu, lakini siwezi kuidharau Singida, wamekuwa na mwenendo mzuri, wanaongoza ligi na ina wachezaji wazuri, haipo hapo kwa bahati mbaya," alisema Gamondi.

Beki wa Yanga, Dickson Job ametabiri kuwa mchezo utakuwa mgumu huenda kuzidi ule wa Coastal Union, kwani si tu kwamba Singida haitotaka kutoka kileleni, lakini ina wachezaji wengi wazuri na wenye ubora kama wao.

"Mchezo utakuwa mzuri na mgumu, kikubwa sisi tunakwenda kupambana ili kupata matokeo mazuri, ushindi wetu uliopita dhidi ya Coastal Union unatupa nguvu ya kuwa tunakwenda kufanya vyema.

Singida ni timu ngumu kwa sababu ina wachezaji bora kama sisi, halafu ikizingatiwa kuwa inaongoza ligi, hawatotaka kutuachia sisi kwenda kileleni kirahisi, kwa hiyo mechi itakuwa ngumu sana kuliko iliyopita, ndiyo maana nasema itabidi tupambane kweli kweli," alisema Job.

Kocha Msaidizi wa Singida, Denis Kitambi, amesema kikosi chake kiko tayari kukabili Yanga, ambapo wanajua wanakwenda kucheza na mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

"Tunajua tunakwenda kucheza na Mabingwa wa Tanzania Bara, na si hivyo tu, bali moja ya timu ngumu kufungika kwa sasa nchini, lakini tumejipanga kukabiliana na hayo yote kwani hata sisi hatujapoteza mchezo wowote kama wao," alisema.

Yanga na Singida, ndiyo timu ambazo hazijapoteza mchezo wowote mpaka sasa kwenye Ligi Kuu, ingawa Singida imeruhusu mabao matatu na Yanga haijaruhu bao lolote.

Timu yoyote itakayofungwa leo itakuwa inapoteza kwa mara ya kwanza na Yanga ikipoteza, itakuwa imeruhusu nyavu zake kuguswa tangu kuanza kwa Ligi Kuu msimu huu.

Ushindi wowote kwa Yanga utaifanya timu hiyo kukwea kileleni na kufikisha jumla ya

INAENDELEA UKURASA 23

# Simba nguvu zote sasa kwa Mashujaa FC

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya mchezo wao wa Ligi Kuu Tanzania Bara uliokuwa uchezwe jana dhidi ya JKT Tanzania kuahirishwa, kikosi cha wachezaji wa Simba kimeendelea na mazoezi mchana wa jua kali kwa ajili ya kwenda kuivaa Mashujaa FC, Ijumaa ijayo kwenye Uwanja wa Tanganyika mkoani Kigoma.

Kikosi hicho kimeendelea na mazoezi yake jana asubuhi hadi mchana wa jua kali na kwa mujibu wa benchi la ufundi, ni kwa ajili ya kuzoea mazingira ya mchezo huo ambao utapigwa saa 10:00 jioni mjini Kigoma.

Kocha Mkuu Fadlu Dalvis, amesema jana kuwa baada ya kuahirishwa kwa mchezo huo, ameendelea kukitengeneza kikosi chake na wachezaji wake waliocheza michezo mingi kupata mapumziko, huku wale majeruhi wakizidi kupata nafuu.

Mchezo huo ulioahirishwa juzi na Bodi ya Ligi kutokana na wachezaji wa JKT Tanzania kupata ajali wakati wakitokea jijini Dodoma kucheza mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Dodoma Jiji, Uwanja wa Jamhuri, Jumamosi iliyopita na kuchapwa bao 1-0.

"Tunaendelea na mazoezi, nadhani baadhi ya wachezaji majeruhi watakuwa wameshapata nafuu, na wengi wenye uchovu watakuwa wamerejea kwenye hali yao ya kawaida, baadhi yao walikuwa

INAENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >